# Nipashe

MWANGA WA JAMII

epaper.ippmedia.com | www.ippmedia.com | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

Alhamisi Novemba 14, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581860

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com


ALIYENUSURIKA KUTEKWA...

# Wanaharakati wapinga polisi kupeleleza mkasa wa jinai

UKURASA 2











" Hii inatuma ujumbe kwa wananchi kwamba vyombo vimeshindwa kupambana na haya makundi ya kuteka watu.

**ONESMO OLE NGURUMWA**

" Jeshi la Polisi linahakikisha linawakamata watu waliokuwa wakijaribu kumwingiza katika gari kama inavyoonekana katika picha mjongeo...

**DCP DAVID MISIME**

" Raia asikubali kukamatwa na watu waliovalia kiraia, wasio na hati ya ukamataji wala kitambulisho cha askari.

**JEBRA KAMBOLE**

KUCHOMA MKE KWA MAGUNIA YA MKAA

## Mawakili wanne watetezi wajitoa wakidai dharau

UKURASA 4

UKURASA WA 3

**Rais** Samia kuhudhuria mkutano wa G20 Brazil



UKURASA WA 3

**Hakimu** agoma kujitoa kwenye kesi ya wanandoa

UKURASA WA 5

**NMB** yawapatia wakulima wa tumbaku bilioni 1.117/- za fidia



## Utata mauaji Katibu wa CCM

UKURASA 2





Skani hapa kutembelea chaneli yetu

## HABARI KITAIFA

# Wanaharakati wang'aka jaribio la kutekwa mfanyabiashara

**Na Restuta James**

WAKATI Jeshi la Polisi likiendelea kuchunguza picha mjongeo iliyosambaa katika mitandao ya kijamii, inayowaonyesha watu watatu wakijaribu kumkamata na kumwingiza kwa nguvu ndani ya gari mfanyabiashara Deogratius Tarimo, wanaharakati wameomba Rais Samia Suluhu Hassan aunde tume ya kiraia kuchunguza matukio hayo.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, aliiambia Nipashe jana kwamba matukio ya 'watu wasiojulikana' kuendelea kukamata watu kwa nguvu yanapaswa kuchunguzwa na tume huru ya kiraia.

"Matukio haya kuendelea kujirudia ni udhaifu mkubwa wa vyombo vyetu vya usalama. Tuna kumbukumbu ya matukio ya watu wametekwa na hawajulikani waliko. Wako waliouawa kama mzee Ali Kibao na hakuna majibu. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba bado yanaendelea kutokea.

"Hii inatuma ujumbe kwa wananchi kwamba vyombo vimeshindwa kupambana na haya makundi ya kuteka watu. Tumeshauri mara kadhaa kwamba njia ya kupambana na matukio haya ni kwa Rais kuunda tume huru ya uchunguzi," alisema.

Olengurumwa alishauri wananchi kujilinda pale wanapovamiwa na kutoa msaada kwa kuwadhibiti wavamizi wanapotaka kumkamata mtu katika eneo lao.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, alisema polisi wanachunguza tukio hilo.

"Jeshi la Polisi linachunguza picha mjongeo inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha watu ambao wanajaribu kumkamata na kumwingiza kwa nguvu ndani ya gari, Deogratius Tarimo ambaye ni mfanyabiashara na mkazi wa Kibaha, mkoani Pwani. Tukio hili liliripotiwa na yeye mwenyewe katika kituo cha Polisi Gogoni jijini Dar es Salaam Novemba 11, 2024," ilisema taarifa hiyo.

Video hiyo ya sekunde 49 ilianza kusambaa juzi katika mitandao ya kijamii, ikimwonesha kijana huyo (aliyetambuliwa kama Deogratius Tarimo), akilazimishwa kuingia kwenye gari aina ya Toyota Raum na vijana wawili.

Kijana huyo alisikika akilia kwamba anakwenda kuuawa na kuomba msaada, huku watuhumiwa wakimwambia watamuua.

"Kulingana na ushahidi uliowasilishwa kituoni hapo na yeye mwenyewe ni kwamba chanzo cha tukio na kilichomsukuma kufika katika hoteli ya Rovenpic iliyoko eneo la Kiluvya, Dar es Salaam, ni kufanya mazungumzo ya biashara," alisema Misime.

Alisema Tarimo amekuwa akiwasiliana na watu hao tangu Oktoba 25, mwaka huu.

"Jeshi la Polisi linahakikisha litawakamata watu waliokuwa wakijaribu kumkamata na kujaribu kumwingiza kwenye gari kama inavyoonekana katika picha mjongeo kulingana na ushahidi ambao umeshakusanywa na unaoendelea kukusanywa ili hatua zingine kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria kwani hakuna aliye juu ya sheria," alisema.

Tukio hilo limeibua mjadala kwenye mitandao ya kijamii, huku wakili Jebra Kambole, akisema raia asikubali kukamatwa na watu waliovalia kiraia, wasio na hati ya ukamataji wala kitambulisho cha askari.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa na viongozi mbalimbali akizindua Jarida la "Sustainable Scalling: Meeting the Clean Cooking Challenges in Africa" wakati wa Mkutano wa kushughulikia Changamoto za Nishati Safi ya Kupikia Afrika: Wito kwa Viongozi wa Afrika, uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29), katika Mji wa Baku nchini Azerbaijan, jana. **Habari Uk. 7.** **PICHA: VPO**


## TANGAZO LA MNADA

**Jackeri, Dc Classic,Held,arm na Makassiwa Kwa idhini tuliyopewa na FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya Mnada Wa nyumba na magari Jijini Dar es saalam, Morogoro,Mwanza na Katoro Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 za hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mteja | Aina ya dhamana | Mahali ilipo | Dalali | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|---|
| 1 Anjela francis malimbwi | Nissa liberty T811 BEP | Dar es salaam | JACKERI | 28.11.2024 |
| 2 COSTANTINE ULIMWENGU NYAMWERU | Mitsubishi pajero T835CCZ | Sumbawamga | DC classic | 28.11.2024 |
| 3 Athuman juma malole | Toyota coaster T188BLK | Dodoma | Held auctioneer | 28.11.2024 |
| 4 Zainabu ali msemo | Mitsubishi Fuso T163CKQ | Arusha | Arm auctioneer | 28.11.2024 |
| 5 Mariam Omary Shango | Plot of land Located at Bugweto and Butengo | Shinyanga | Mkassiwa | 28.11.2024 |
| 6 Seleman Ramadhan Mkuga | Plot of Land Located at Mongolo-Kahama | Shinyanga | Mkassiwa | 28.11.2024 |
| 7 Hilda Masumbuko Ndekeja | House located in Tinde | Shinyanga | Mkassiwa | 28.11.2024 |
| 8 Asma Mwandu Mitayo | House Located in DIDIA | Shinyanga | Mkassiwa | 28.11.2024 |
| 9 Fredy Stanslaus Muma | Plot of Land Located at NGOKO | Shinyanga | Mkassiwa | 28.11.2024 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya Tangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga 0677014355 (Fanikiwa)**


# Utata mauaji Katibu wa CCM

**Na Francis Godwin,** IRINGA

UTATA umeibuka katika tukio la mauaji ya kinyama ya Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, Christina Kibiki (56), wajukuu wake wakidai kuwa kabla ya bibi yao kuuawa, alibakwa sebuleni kisha kuingizwa chumbani alikouliwa kwa kitu chenye ncha kali.

Asifiwe Kibiki, mmoja wa mashuhuda wa mauaji hayo, alidai kuwa wauaji hao walikuwa zaidi ya watatu, mmoja aligonga mlango kuwa ana shida na bibi yao.

"Baada ya kugonga mlango, walimwulizia bibi na wakati bibi anatoka nje kwenda kumsikiliza, ghafla walimgeuzia kibao na kuanza kumshambulia na kumvutia ndani, dada yangu alipojaribu kumsaidia alipigwa na kuanguka chini," alidai.

Shuhuda huyo alidai kuwa baada ya dada yake kuanguka chini, mtu huyo wasiyemjua, alimvutia ndani bibi yao na kuanza kumbaka na wakati huo wao walikimbia nje kupiga kelele kuomba msaada.

Alidai kuwa aliyekuwa anatenda ukatili kwa bibi yao, alikuwa na silaha mfukoni yenye mfanano na bastola, hali iliyowafanya kuogopa zaidi.

"Huyu mtu mmoja aliyekuwa akimbaka bibi, aliingia ndani pekee yake ila nje wenzake wawili walikuwa wakiimarisha ulinzi mmoja, alikuwa akinywa soda na mwingine akitazama watu ila sijui kama baadaye wote waliingia ndani," alidai.

Shuhuda huyo alidai kuwa baada ya kumfanyia ukatili huo sebuleni bibi yao, walimvutia chumbani kwake na kuanza kumchoma na vitu vyenye ncha kali kisha kumtupa kwenye boksi lililokuwa chumbani kwake.

Shuhuda huyo alimweleza mwandishi wa habari hizi aliyefika jana katika kitongoji cha Banawano, kijiji cha Ugwachanya, kata ya Mseke, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kupata undani wa tukio hilo lililotokea juzi saa tatu usiku wa Novemba 12 mwaka huu.

Ni tukio hilo lililoacha simanzi kwa familia, majirani na viongozi wa chama.

Kwa mujibu wa Asifiwe Kibiki, mjukuu wa marehemu, Christina alivamiwa na kijana ambaye hakutambulika mara moja.

Asifiwe alidai kuwa mvamizi huyo aliingia ndani ya nyumba kwa ghafla na kufanya unyama huo kisha kumwacha bibi yake akiwa hoi.

"Baada ya shambulio, tulisikia mlipuko kama bomu, na majirani walikusanyika kwa ajili ya kutoa msaada, lakini watuhumiwa walikuwa tayari wametoroka," aliongeza.

Festo Mwangamila, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Banawano, alisema kuwa alipofika eneo la tukio baada ya kupigiwa simu, watuhumiwa walikuwa wameshatoweka.

"Tukio hili ni la kwanza kutokea katika kitongoji chetu na limeleta hofu kubwa," alisema Mwangamila.

Laula Kilienyi, Diwani wa Viti Maalumu Tarafa ya Mlowe, akimzungumzia Christina, alimtaja kama kiongozi shupavu, mchangamfu na mpenda watu.

"Atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya jamii na uongozi bora," alisema Diwani Kilienyi aliyekuwa anazungumza kwa huzuni.

Shakila Kiwanga, Diwani wa Kalenga, alielezea jinsi alivyopokea taarifa za tukio hilo saa tano usiku kutoka kwa mtoto wa marehemu. Alifuatilia haraka mkasa huo hadi Hospitali ya Tosa Maganga, ambako alikuta Christina akiwa na hali mbaya kiafya.

"Lakini baada ya muda mfupi, tulipata taarifa za kifo chake, jambo lililotuuma sana," aliongeza Kiwanga.

Wakati mjukuu wa marehemu huyo akidai bibi yake alibakwa kabla ya kifo chake, Dk. Thomas Malongo, Mkurugenzi wa Tiba katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Tosa Maganga), alisema walimpokea Christina akiwa hajitambui, huku akiwa na majeraha mengi mwilini na kuvuja damu puani na masikioni.

Alisema kuwa Christina amepoteza maisha kutokana na majeraha mawili ya vitu vyenye ncha kali na kuwa hawawajaona dalili za kubakwa.

"Madaktari walijitahidi kuokoa maisha yake kwa kuzuia damu kuvuja zaidi, lakini isivyo bahati alifariki dunia baada ya saa moja na nusu," alisema Dk. Malongo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, SACP Allan Bukumbi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa uchunguzi unaendelea ili kubaini wahusika.

"(Christina) alipigwa risasi kifuani na kitu kizito kichwani, na watuhumiwa walitoroka bila kuchukua kitu chochote nyumbani kwa marehemu," alisema Kamanda Bukumbi.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi kutoa taarifa zozote zitakazosaidia kukamatwa kwa wahalifu hao ili kuhakikisha haki inatendeka.

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email: customerrelations@guardian.co.tz**

HABARI KITAIFA

# Hakimu agoma kujitoa kesi ya wanandoa

**Na Grace Gurisha**

HAKIMU Mkazi Mkuu Aaron Lyamuya wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, amekataa kujitoa kusikiliza kesi ya madai ya kujeruhi inayowakabili Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54) kwamba hakuna sababu ya msingi iliyotolewa na upande wa utetezi.

Aidha, amesema amekuwa akiwakubalia watu kujitoa katika kesi zao ambao hawana mawakili mahakamani kwa sababu hawana uwelewa wa sheria lakini sababu iliyotolewa na Wakili Mkongwe, Gabriel Mnyele, haina mashiko.

Hakimu Lyamuya alitoa uamuzi huo mdogo jana baada ya mawakili wa washtakiwa hao, Mnyele na Edward Chuwa, kuomba ajitoe kwa madai amewakatalia mapingamizi yao mawili wakati kesi hiyo inasikilizwa kwa mashahidi wa upande wa Jamhuri.

"Katika hoja hizi zilikuwa za upande mmoja tu za Wakili Mnyele. Hili suala si geni la kutaka hakimu au jaji kujitoa kwenye kesi. Ni mambo ya kawaida lakini unatakiwa utoe sababu za msingi za kisheria na si hisia tu.

"Ikiwa sababu zitaonesha kwamba kuna haki haitotendekeka au upendeleo wowote au una rafiki au ndugu kwenye kesi basi unajitoa. Katika maelezo ya Mnyele, nilitarajia haya anayajua angeeleza sababu za msingi.

"Ingekuwa hoja hii imeletwa na mtu wa mtaani asiyejua sheria, ningefikiria kujitoa lakini kwa mtu 'senior' (waandamizi) kama Mnyele, siwezi kujitoa kwa kuwa hakuna sababu za msingi,"alisema.

Aliendelea kusema: "Kuwakatalia mapingamizi si sababu bali walitakiwa kutafuta wapi walikosea na si kuhamaki. Hawafanyi uamuzi kwa hesabu kwa sababu nimewakatalia mara mbili basi ndiyo atoe uamuzi tofauti hiyo haiwezekani.

"Ningekuwa nafanya hivyo kwa kutoa uamuzi kwa namba ningekuwa nafanya sijakaa kwenye kiti hiki. Kesi nitaendelea nayo mimi hadi mwisho. Kama mtakuwa hamjaridhika hadi mwisho mtakata rufani kwamba nilikataa kujitoa ila si sasa."

Baada ya kumaliza kutoa uamuzi wake, Wakili Chuwa alianza kuzungumza kile ambacho alizungumza Mnyele ndipo akamhoji anataka afanye nini wakati tayari ameshatoa uamuzi na kwamba anapanga tarehe ya shauri kuendelea kusikilizwa.

Baada ya hakimu kusema hayo, Wakili Chuwa alimgeukia hakimu na kumweleza kwamba kwa nini anazungumza kwa jazba. Hakimu Lyamuya alimjibu kwamba: "Mimi sijaongea jazba, nimekueleza kwamba napanga tarehe nyingine ya kusikiliza. Hiyo jazba inatoka wapi wakati tayari nimeshatoa uamuzi?

"Kwanza hata tai hajavaa hauko 'proper' (sawa) halafu unazungumza vitu ambavyo havipo. Hapa kuna wanafunzi wa sheria watajifunza nini kutoka kwako? Haya nipange tarehe ngapi kesi?"

Kesi imeahirishwa hadi Desemba 3,2024 saa 5:00 asubuhi na shahidi namba tano

Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Calvin (36) ataendela kutoa Ushahidi wake. Awali, shahidi huyo, hakumaliza kutoa ushahidi wake kutokana na ubishani uliotokea kwa Wakili Mnyele kudai kuwa hawezi kuelezea kile alichokiona kwenye kamera za CCTV kwa sababu ni suala la kieletroniki.

Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania wenye asili ya Kiasia wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana, Dar es Salaam, wanakabiliwa na mashtaka manne waliyoyatenda Julai 21,2023 kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa Nathwan, Julai 21 ,2023 akiwa eneo la mtaa wa Mrima-Kisutu, jengo la Lohana, kinyume cha sheria, alimsababishia madhara makubwa Kiran Lalit kwa kuzamisha kichwa chake kwenye ndoo ya saruji iliyochanganywa.

# Samia kuhudhuria mkutano wa G20 Brazil

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajia kushiriki mkutano wa viongozi wa G20 utakaofanyika Rio de Janeiro, Brazil kwa siku mbili kuanzia Novemba 18, mwaka huu.

Mkutano huo umebebwa na kaulimbiu isemayo: "Kujenga Ulimwengu wa Haki na Sayari Endelevu".

Mwaliko huo umetolewa na Rais wa Brazil, Luiz Inacio Lula da Silva, na Rais Samia atakuwa Rais wa kwanza mwanamke kuwahi kuhudhuria mkutano wa viongozi wa G20.

Pia ni Rais wa kwanza wa Tanzania kuhudhuria mkutano huo wa viongozi wa G20 tangu kupanuka kwa kundi hilo kutoka G8 hadi G20 mwaka 2009.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, historia inaonesha kuwa Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa na Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, walishiriki mikutano ya G8 iliyofanyika mwaka 2005 na 2008 mtawalia.

Ushiriki huo wa Rais Samia katika mkutano wa viongozi wa G20 unaashiria kuongezeka kwa ushawishi na mwonekano wa Tanzania katika jukwaa la kimataifa.

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo, katika mkutano wake jana na mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao nchini, aliwahakikishia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, unaotarajia kufanyika Novemba 27, mwaka huu, utakuwa huru, haki na wenye uwazi zaidi.

"Tunapojiandaa na mchakato huu muhimu wa kidemokrasia, serikali ilifanya kampeni kuhusu uandikishaji wapiga kura kwa nia ya kuhakikisha kila mwananchi anayestahili wakiwamo wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum wanapata fursa na nafasi ya kujiandikisha na kutekeleza haki zao za msingi za kikatiba," alisema.

Kadhalika alisema Sera ya Mambo ya Nje iliyofanyiwa marekebisho ijulikanayo kama Toleo la 2024 imekamilika na hivi karibuni na itachapishwa rasmi na kupatikana kwa wadau wote.

Alisema sera hiyo itaendelea kuweka mkazo katika diplomasia ya uchumi na katika kanuni zilizopo za kulinda maadili ya kijamii. Pia alisema inakuja na masuala ya ziada katika nyakati za kisasa ikiwa ni pamoja na matumizi ya Lugha ya Kiswahili kama nyenzo madhubuti ya diplomasia ya nchi.


AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
benki kwa maendeleo yako

## TAARIFA KWA UMMA

### Akiba Commercial Bank Plc kufanya Maboresho ya Mfumo Mkuu wa Kibenki

Tunapenda kuwajulisha wateja wetu wote, washirika na umma kwa ujumla kuwa benki imeboresha mfumo wake mkuu wa kibenki ili kuleta ufanisi zaidi katika upatikanaji wa huduma za kibenki .

Utekelezaji rasmi utaanza, **Jumatatu, tarehe 18 Novemba 2024.** Aidha katika mchakato wa maandalizi tunapenda kuwafahamisha wateja kuwa **Jumamosi na Jumapili, tarehe 16 na 17 Novemba 2024** huduma zote za kibenki zikiwemo huduma ya benki mtandaoni (internet Banking), huduma ya benki kupitia simu ya mkononi (Akiba Mobile) ATM kadi za Umoja na VISA, huduma za mawakala na matawi hazitapatikana kwa siku mbili hizo. Tunawashauri wateja kufanya utaratibu wa kupata mahitaji yao ya kibenki ya lazima kwa kufanya miamala yao mapema kabla ya kipindi hicho.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na timu yetu ya huduma kwa wateja kwa namba **+255 746 811 510** au kupitia barua pepe **info@acbbank.co.tz.**

**Menejimenti**
**Akiba Commercial Bank Plc**



Washtakiwa wa kesi ya uhujumu uchumi ya kusafirisha vipande 660 vya meno ya tembo vyenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4.6, wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kusikiliza kesi inayowakabili, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

KUCHOMA MKE KWA MAGUNIA YA MKAA

# Mawakili wa utetezi wajitoa katika kesi

**Na Grace Gurisha**

JOPO la mawakili wanne wanaomtetea mfanyabiashara Khamis Luwongo (38) anayetuhumiwa kumuua mkewe Naomi Marijani na kisha kuuchoma moto mwili wake kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, wamejitoa kumtetea kwa madai anawadharau na hawaheshimu.

Vilevile, mshtakiwa Luwongo amedai hawezi kuwalazimisha kwa sababu anayeteseka ni yeye wao, wanarudi nyumbani kulala na wake zao, huku akirudishwa gerezani, ndiyo maana wanaomba tu mapumziko ya kutaka kwenda kula.

Mawakili hao, Mohamed Majaliwa, Mikidadi Zidadi, Fatuma Abdul na Jaquim Kamuli, waliomba juzi mbele ya Jaji Hamidu Mwanga wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kujiondoa baada ya mshtakiwa kutokuwa na imani nao.

Luwongo alifikia hatua hiyo baada ya Wakili wake, Majaliwa kuomba mahakama mapumziko kidogo kama ya dakika 30 kwa sababu kesi ilianza kuanzia saa 4:42 asubuhi hadi saa 7:12 mchana bila mapumziko, lakini mshtakiwa hakukubaliana na suala hilo.

Mshtakiwa alinyoosha mkono mbele ya Jaji Hamidu Mwanga, na alipotakiwa asimame na kuzungumza, alidai kuwa anaona mawakili wake hawako makini na kesi yake, hivyo anaomba mahakama asimame mwenyewe kujitetea.

"Mawakili wangu hawako 'serious', kama wao wamechoka mimi niendelee mwenyewe. Ni kesi ya muda mrefu, wao wanataka kwenda nyumbani, mimi ninakwenda gerezani, break (mapumziko) ya nini, waseme wameshindwa niulize mwenyewe maswali kwa mashahidi," alidai Luwongo.

Baada ya mshtakiwa kudai hayo, Wakili Majaliwa alidai kuwa hawezi kumwudhi bosi wake, kwa hiyo waendelee na shahidi wa upande wa mashtaka.

Jaji Mwanga alimtaka Wakili wa Serikali Mkuu Yasinta Peter azungumze naye kuhusu hoja hizo, alibariki hoja ya mapumziko kidogo kwa sababu kuna wengine wanaumwa, wanakunywa dawa na wengine wagonjwa wa kisukari, wanahitaji mapumziko.

Baada ya hoja hizo, Jaji Mwanga alimwita shahidi mara tatu kwa kumtaka asimame juu, lakini hakusikia ndipo aliposimama jaji akamwuliza 'shida nini?'. Akadai kuwa mawakili wake wanamchanganya.

"Usichanganyikiwe, hii kesi inaisha, tupate mapumziko kidogo turudi hapa ndani saa 8:50 mchana," alisema Jaji Mwanga.

Baada ya ahirisho hilo, mshtakiwa Luwongo alitoka kizimbani kwa hasira akielekea nje huku akimwelekeza askari magereza kwamba waondoke.

Ilipofika saa 9:21 mchana, mahakama ilianza tena baada ya mapumziko, Wakili Peter alieleza mahakama kwamba hakuna kilichobadilika, jopo ni lilelile, wakamwita shahidi ili waendelee na usikilizwaji.

Baada ya Jaji kumwuliza Wakili Majaliwa kwa upande wao, alianza kwa kuomba radhi kwamba mahakama haiwezi kuendelea na kesi hiyo kwa sababu tayari mteja wake ameonesha kutokuwa na imani naye, na pia alidai ifikie hatua mawakili waheshimike.

"Samahani sana Mheshimiwa Jaji, mimi siwezi kuendelea, mteja wangu ameonesha dharau na pia hatuheshimu, anasema hatupo 'serious' wakati nimeacha shughuli zangu zote nipo hapa, kuna kesi yangu Mahakama ya Temeke imefutwa kwa sababu ya kesi hii.

"Ifikie hatua wateja wetu watuheshimu, mimi siwezi kuendelea, nimekaa naye gerezani zaidi ya mwaka mmoja halafu anasema mimi sijui maumivu ya mahabusu, amenikosea sana, siwezi kuendelea naye," alidai Wakili Majaliwa.

Wakili Mikidadi naye akasimama, akaeleza mahakama kwamba anaomba ajiondoe kwa sababu amechoka na dharau za mteja wao na pia ameonesha kutowaamini.

"Mheshimiwa Jaji, siwezi kuendelea, nimechoka na hiki anachokifanya mteja wetu, hatuamini! Mimi mwenyewe kwa sasa simwamini," alidai Wakili Abdul kwa upole sana kuonesha hajapendezwa na kitendo alichokitenda mteja wao.

Naye Wakili Kamuli ambaye alipangwa na mahakama kumtetea mshtakiwa huyo, pia aliomba ajitoe kwa madai kuwa mshtakiwa hana imani naye, isije ukatoka uamuzi akadai wao ndiyo wamesababisha.

"Mnajua ninyi ni maofisa wa mahakama, mnatakiwa kuisaidia. Kama mnataka niwatoe, ninataka mshtakiwa mwenyewe aseme kwani yeye amewakataa? Unajua suala hili ni kunyongwa hadi kufa na huyu ni shahidi wa 12?" alisema Jaji Mwanga.

Baada ya hoja hiyo, Jaji Mwanga alimgeukia Mshtakiwa Luwongo na kumwuliza kama amewakataa mawakili, akadai kwamba hana haja ya kuwabembeleza, waondoke kwa sababu kuna mawakili wengi tu wanakwenda gerezani kutaka kumtetea.

Baada ya Jaji kusikiliza hoja hizo, aliwaondoa mawakili hao katika kesi hiyo kama walivyoomba. Kesi imeahirishwa hadi Novemba 18 mwaka huu, mshtakiwa amepewa muda wa kutafuta wakili, lakini alisisitiza anataka kujitetea mwenyewe.

Mshtakiwa Luwongo ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kuwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole, Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

## TAKUKURU yakusanya mamilioni katika leseni za biashara, ushuru wa huduma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma imekusanya Sh. milioni 308.6 ndani ya siku 10 baada ya kuendesha msako wa makusanyo yatokanayo na leseni za biashara, ushuru wa huduma na ushuru wa mabango kwa wafanyabiashara wa kata za Madukani, Uhuru na Majengo za jijini.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Victor Swella, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa robo ya kwanza ya mwaka huu.

Alisema msako huo ulifanyika kwa ushirikiano wa ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma. Kati ya fedha hizo, Sh. milioni 107.5 ni za leseni ya biashara na Sh. milioni 194.8 zimetokana na ushuru wa huduma, huku Sh. milioni 6.2 zikitokana na ushuru wa mabango.

Alisema msako huo umetokana na TAKUKURU kupata taarifa za kuwapo watu wanaofanya biashara bila kuwa na leseni na wengine wanakwepa kulipa ushuru sahihi kwa Halmashauri ya Jiji.

"Tulianza ufuatiliaji katika kata hizi tatu na kukusanya kiasi hicho cha fedha na tutaendelea na zoezi hili katika maeneo mengine ya biashara, lengo ni kutaka kila mmoja alipe ushuru sahihi, na wafanyabiashara wafanye biashara wakiwa na leseni ili kuepuka upotevu wa mapato," alisema Swella.

Alisema TAKUKURU pia imebaini upungufu katika miradi 40 yenye thamani ya Sh. bilioni 6.3 kati ya miradi 58 ya maendeleo inayotekelezwa mkoani Dodoma, ikiwamo ya uboreshwaji miundombinu ya shule za msingi na sekondari.

Swella alisema taasisi hiyo inaendelea na ufuatiliaji wa miradi hiyo na kutoa ushauri wa namna bora ya kurekebisha upungufu uliopo na kuchukua hatua za kudhibiti mianya ya rushwa.

Swella pia alisema taasisi hiyo imepokea malalamiko yenye viashiria vya rushwa kutoka kwa wagombea wa nafasi mbalimbali za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alisema malalamiko mengi ni yale ya wagombea kukatwa majina na kuongeza kuwa taasisi hiyo imerejesha suala hilo kwa vyama husika vya siasa.

Swella alisema moja ya vipaumbele ambavyo TAKUKURU wamejiwekea ni pamoja na kuongeza kasi ya uelimishaji umma kuhusu madhara ya rushwa katika uchaguzi na ufuatiliaji utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo.

## Shahidi abanwa kwa hoja za kisheria Korti ya Mafisadi

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa upande wa mashtaka, Rabson Mosha amebanwa na hoja za kisheria, akidaiwa kachukua maelezo ya onyo kwa mshtakiwa Ziada Salumu bila kumweleza hatari na adhabu atakayopewa kwa kukiri kusafirisha kilo 7.26 za dawa za kulevya.

Hayo yalijiri jana Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu, maarufu Mahakama ya Mafisadi, mbele ya Jaji Monica Otaru wakati shahidi wa upande wa mashtaka akitoa ushahidi wake.

Shahidi alidai kwamba, mwaka 2021 alikuwa ofisa wa polisi mwenye namba G4350 Koplo Rabson na alikuwa anafanya kazi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere akiwa mpelelezi wa makosa ya jinai.

Alidai alifanya kazi kituoni huko kwa miaka minne na Desemba 19, 2021, akiwa kazini alipewa jukumu la kuandika maelezo ya onyo la mshtakiwa Ziada.

Alidai alimfahamisha haki zake, akidai kuwa mshtakiwa huyo alikamatwa maeneo ya Kinyerezi Desemba 19, 2021 saa tatu usiku akiwa na mabegi mawili yenye dawa za kulevya.

"Mshtakiwa katika maelezo yake alikiri kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya, alifuata dawa hizo Zambia, akazileta Dar es Salaam na kuwakabidhi washtakiwa wengine Salum Athumani na Saidi Musa. "Mheshimiwa, ninaomba kuyatoa maelezo ya onyo yenye saini na dole gumba la mshtakiwa kama sehemu ya ushahidi wangu mahakamani," alidai shahidi.

Wakili wa Utetezi, Hekima Mwasipo akijibu kuhusu maombi hayo, alidai maelezo yaliandikwa kinyume cha sheria kwa sababu sheria inataka mwandikaji maelezo aandike muda katika kila kipengele cha onyo. Alidai maelezo yanayoombwa kutolewa, yana kasoro kwa kuwa hakuna sehemu iliyoandikwa muda na pia mshtakiwa alitakiwa kuonywa kuhusu hatari atakayokutana nayo.

"Mshtakiwa anatakiwa aambiwe kifungu na sheria inayotumika kumpa onyo pamoja na adhabu atakayokutana nayo akikiri makosa anayotuhumiwa," alidai Mwasipo. Alidai katika maelezo yaliyopo, hakuna mahali ambako mshtakiwa alionywa kuhusu adhabu atakayopata endapo akikiri kosa.

Wakili Mwasipo alidai maelezo yote anayoomba shahidi kuyatoa mahakamani, hayana kifungu cha sheria na kukosekana kwa vifungu vya sheria ni sawa na hakuna maelezo.

Alidai maelezo hayakutolewa kwa ridhaa ya mshtakiwa kwa kuwa kulikuwa na vitisho, mshtakiwa alipigwa na kulazimishwa kutia saini na kuweka dole gumba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Itike Mwaisaka alipotakiwa kujibu, alidai maelezo ya onyo yanayoomba kutoa yaliandikwa chini ya sheria ya dawa za kulevya. Alidai maelezo hayo yalizingatia taratibu zilizoelekezwa katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA). "Suala la kuandika muda katika kila kipengele cha onyo kisheria halihitajiki katika fomu ya maelekezo ya kuchukua maelezo ya onyo.

"Hoja ya kwamba mshtakiwa alitakiwa kuelezwa hatari atakayokutana nazo kwa kukiri kosa, wakili hakusema kifungu gani cha sheria kinaelekeza hivyo, mshtakiwa anachopaswa kuelezwa ni madhara yatakayotokea baada ya kutoa maelezo yake," alidai Itike.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili iliruhusu kuingia kesi ndani ya kesi kwa ajili ya kusikiliza ushahidi wa mshtakiwa kuhusu madai kwamba alitishwa, alipigwa na kulazimishwa kutia saini maelezo ya onyo.

Baada ya kusikiliza kesi ndani ya kesi, mahakama itapanga kutoa uamuzi wa ama kupokea au kukataa kupokea maelezo ya onyo ya mshtakiwa kama ushahidi wa upande wa mashtaka.

Wakati huo, mahakama hiyo mbele ya Jaji Godfrey Isaya iliahirisha kutoa uamuzi wa kupokea au kukataa kielelezo cha kilo 126.36 za bangi katika kesi inayomkabili Juma Bakari kwa sababu jaji ana udhuru. Uamuzi utatolewa kwa tarehe itakayopangwa na mahakama.

# Mwanafunzi adaiwa kughushi nyaraka za mil.30/- mradi ujenzi barabara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Shinyanga, imebaini ubadhirifu wa fedha katika ujenzi wa barabara ya Isoso-Mwabusiga yenye urefu wa kilomita tatu wilayani Kishapu, huku mwanafunzi aliyeko kwa mafunzo ya vitendo, akidaiwa kughushi nyaraka za ujenzi wa barabara hiyo, yenye thamani ya Sh. milioni 29.1.

Kaimu Kamanda wa TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga, Mwamba Masanja, alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari ya kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba, 2024.

Alisema kwa kipindi hicho wameshughulikia tatizo la ubovu wa barabara hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 29.1 na kubaini ubadhirifu wa fedha na kuwa nyaraka za barabara hiyo zilighushiwa.

Barabara hiyo, alisema ilikuwa inakarabatiwa na Advance Construction Ltd chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wilayani Kishapu ambayo ilikuwa imejengwa chini ya kiwango. Alisema katika ufuatiliaji wao walibaini upungufu katika ushindiliaji wa kifusi kuwa chini ya viwango vya ubora, huku mkandarasi akilipwa pesa zote za mradi.

Masanja alisema TAKUKURU ilielekeza TARURA kumsimamia mkandarasi aifanyie marekebisho barabara hiyo ili thamani ya fedha ionekane lakini maelekezo hayo yalipuuzwa.

"Baada ya kuona maelekezo yetu kutofanyiwa kazi, tulifanya uchunguzi wa kina juu ya barabara hiyo na kubaini kughushiwa kwa nyaraka za matokeo ya vipimo vya ubora vya barabara hiyo, vikionyesha ushindiliaji umekidhi viwango jambo ambalo si sahihi," alisema.

Masanja alisema nyaraka hizo zilighushiwa, kuandaliwa na kusainiwa na Mhandisi aliyekuwa mafunzoni (trainee engineer) kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Shinyanga, ambaye hakuwa na jukumu hilo huku mkandarasi akiwa ameshalipwa pesa zote.

Pia alisema baada ya uchanguzi kukamilika, watuhumiwa watatu walifikishwa mahakamani. Watuhumiwa hao ni Juma Mkela aliyekuwa msimamizi wa kampuni ya ujenzi, Charles Emmanuel mhandisi mwanafunzi na Wilfred Gutta, Meneja wa TARURA Wilaya ya Kishapu na wote walikiri makosa kwa matumizi mabaya ya mamlaka na kughushi nyaraka.

Alisema baada ya kutiwa hatiani, mahakama ilitoa adhabu kwa kila mtuhumiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 pamoja na kurejesha fedha yote serikalini ya ujenzi wa barabara hiyo na kwamba faini ililipwa Sh. milioni 2.5, na kurejesha Sh. milioni 10 na kusalia milioni 19.1 ambazo alilipwa mkandarasi isivyo halali. Katika hatua nyingine, Masanja alisema taasisi hiyo imeendelea kudhibiti vitendo vya rushwa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu, kwa kutoa elimu ya rushwa kupitia majukwaa na mikutano mbalimbali.



Kaimu Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Shinyanga, Mwamba Masanja (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jana, kuhusu taasisi hiyo, kubaini ubadhirifu wa fedha kwenye ujenzi wa barabara ya kilomita 3 ya Isoso-Mwabusiga, wilayani Kishapu, yenye thamani ya Sh. milioni 29.1. **PICHA: MARCO MADUHU**

## NMB yawapatia wakulima wa tumbaku bil. 1.117/- za fidia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amepongeza Benki ya NMB kwa kukabidhi fidia ya Sh. bilioni 1.117 kwa wakulima wa tumbaku 2,226 kutoka Vyama vya Msingi (AMCOS) 22 mkoani Tabora waliokopa katika taasisi hiyo iliyotenga zaidi ya Sh. bilioni 291 za mikopo ya kilimo cha zao hilo kwa msimu wa 2024/25.

Bashe alitoa pongezi hizo jana wakati akipokea hundi ya mfano kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, naye kuikabidhi kwa Mwakilishi wa Wakulima na Mwenyekiti wa AMCOS ya USAGUZI, Ally Mrisho, mbele ya Dk. Baghayo Saqware, Kamishna wa Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA).

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Waziri Bashe alisema NMB na Kampuni ya Bima ya UAP wameonesha mfano wa kuigwa kwa kukubali kuchukua hatari na kutoa bima za kilimo, sekta aliyoitaja kuwa ngumu zaidi kukopesheka kutokana na wingi wa vihatarishi vinavyoizunguka sekta na wadau wake, hasa wakulima.

"Kuthibitisha dhamira ya dhati ya NMB katika kukuza sekta ya kilimo, ilitoa mikopo yenye thamani ya dola milioni 60, takribani Sh. bilioni 150 hivi. Jumla ya AMCOS 256 zilinufaika na mikopo hiyo, lakini athari zikawafikia wakulima kutoka AMCOS 22, wanaolipwa fidia hii kutoka NMB na UAP.

"NMB wamekuwa vinara wa utoaji fidia za bima za kilimo na kila mmoja hapa anafahamu kwamba hakuna sekta ngumu kukopesheka kama kilimo, kutokana na vihatarishi vya sekta hiyo, lakini NMB na UAP wamesimama imara kuhakikisha wakulima wanaelewa umuhimu wa bima hizi.

"Serikali tumejipanga katika kufanikisha 'Comprehensive Agricultural Scheme,' bila hiyo hakuna mkulima anayeweza kukopesheka, TIRA iharakishe mchakato huo, kwani kila zao lina tabia zake na vihatarishi vyake na serikali inajipanga kuhakikisha tunajenga mfumo wa bima kwa kila zao kulingana na vihatarishi vyake," alisema.

Bashe alibainisha ya kwamba tumbaku imekuwa zao muhimu kwa uchumi wa taifa na kuwa miaka mitatu nyuma, Tanzania haikuwa mzalishaji mkubwa, lakini kutokana na mchango wa taasisi za fedha, zikiongozwa na NMB, sasa Tanzania ni ya pili kwa uzalishaji tumbaku Afrika.

Aliongeza kwamba, licha ya athari zilizolipiwa fidia hiyo ya bilioni 1.117, mapato ya jumla ya zao la tumbaku kwa msimu wa 2023/24 yalikuwa Sh. bilioni 724 kutoka Sh. bilioni 717 za msimu wa 2022/23 na kwamba msimu huu wa 2024/25, matarajio ya pato la jumla kwa wakulima litakuwa Sh. trilioni 1.7.

Akizungumza katika hafla hiyo, Zaipuna alisema licha ya kukabidhi hundi yenye thamani ya Sh. bilioni 1.117 ikiwa ni fidia kwa wakulima wa tumbaku na Vyama vya Ushirika na Masoko (AMCOS) mkoani Tabora waliokopa katika benki hiyo, NMB imetenga Sh. bilioni 291.6 kwa ajili ya mikopo ya kilimo hicho msimu huu.

Alisema wakulima hao walikatia bima mikopo yao kwa UAP, na hiyo ni mara ya pili kwa NMB na UAP kutoa fidia ya bima kwa wakulima wa tumbaku wa mkoa wa Tabora, ambapo mwaka jana walikabidhi fidia ya Sh. milioni 374 kwa wakulima 400 kwa sababu hizo hizo za hali ya hewa kuathiri kilimo chao.

"Wakulima tunaowafidia leo (jana) ni mmoja mmoja na ambao kupitia AMCOS zao, walichukua mikopo ya kilimo cha Tumbaku NMB, ambayo ilikuwa na bima kutoka kampuni hii na hili linakuja baada ya kukamilisha upembuzi na tathmini thabiti na washirika wetu hao," alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Uamuzi kurejesha wagombea walioenguliwa wa kupongezwa*

**TANGU** kuanza kwa mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu, kumekuwa na mivutano ya hapa na pale ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa inahatarisha mazingira ya kutokuwa huru na haki.

Mivutano hiyo ilianza wakati wa uandikishaji wa wapiga kura katika Daftari la Makazi, kura za maoni ndani ya vyama na uteuzi wa wagombea kupitia vyama na baina ya vyama vya siasa. Aidha, mambo hayo yalisababisha kasoro kubwa na hata kuweka taswira ya kutokuwapo kwa amani, umoja na mshikamano ndani ya jamii.

Kubwa zaidi, kama wahenga wasemavyo mwanzo wa ngoma ni kelele, ngoma kamili ilionekana kupigwa wakati wa uteuzi wa wagombea watakaowakilisha vyama kwenye uchaguzi huo. Ngoma hiyo ilihusu kuenguliwa kwa wagombea huku vyama vya upinzani vikilia zaidi kwamba ndivyo vilivyoathirika na sakata hilo.

Vilio vilisikika kila kona ya nchi kutoka vyama vya upinzani hasa vile vinavyoonekana vinaweza kutoa ushindani dhidi ya chama tawala - Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwenye uchaguzi huo katika baadhi ya maeneo. Vyama hivyo ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ACT - Wazalendo na Chama cha Wananchi (CUF).

Kwa mujibu wa baadhi ya viongozi wa vyama hivyo, wagombea wao waliondolewa katika kugombea nafasi za uenyeviti wa mitaa, vijiji, vitongoji na ujumbe wa serikali za mitaa kwa madai ya kukiuka kanuni na taratibu. Viongozi hao walidai kuwa hizo zilikuwa njama za CCM kwa kushirikiana na viongozi waliopewa dhamana ya kuendesha mchakato wa kupitisha wagombea kabla ya kuanza kampeni na hatimaye uchaguzi.

Miongoni mwa kasoro zilizobainishwa na maofisa wenye dhamana ya uteuzi wa wagombea ni kukosea kujaza fomu na kushindwa kupata muhuri wa chama husika ili kuthibitisha kama wamedhaminiwa na vyama vyao. Sababu zingine zilizotolewa ni baadhi ya wagombea kutokuwa wakazi wa maeneo husika, kudaiwa kuwa wajasiriamali jambo ambalo lilielezwa kuwa si kazi ya kumpa mtu kipato. Pia ilidaiwa kuwa hata walipoambiwa kuwa wagombea wenye malalamiko wawasilishe rufani zao kwa siku zilizopangwa, walikuta ofisi zikiwa zimefungwa, hivyo kuwanyima nafasi ya kutumia haki zao kwa jambo hilo.

Hata hivyo, serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilikanusha madai ya viongozi hao kwamba wanazusha hoja hizo huku Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, alisema wapinzani wanatafuta huruma kwa mambo ambayo hayapo.


Kutokana na kuwapo kwa sintofahamu hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, aliagiza TAMISEMI kuwaruhusu wale walioenguliwa kwa kasoro ndogondogo, warejeshwe na kugombea huku Mchengerwa naye akiongeza muda wa kukata rufani na kuweka mapingamizi baada ya siku zilizowekwa kumalizika.

Kwa ujumla, hatua iliyochukuliwa na Rais Samia ni ya kuigwa kwa sababu ameepusha mambo mengi ambayo yangetia doa taifa hasa katika jumuiya ya kimataifa kuwa kinachozungumzwa si kile kinachotendeka. Rais ameonyesha kwa vitendo kuwa hataki kuona mambo yasiyo ya kidemokrasia, uhuru na haki yakiendelea kutendeka kama ambavyo imekuwa ikilalamikiwa kwa kutolea mfano wa uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Rais Samia tangu ameingia kwenye nafasi hiyo mwaka 2021, aliweka bayana kwamba Watanzania wanapaswa kuwa wamoja huku wakiheshimiana na kupendana ndiyo maana alianzisha falsafa ya 4R ili kurejesha demokrasia na uhuru wa kujieleza ambao ulidaiwa kuwa viliminywa wakati wa mtangulizi wake.

Kama alivyoagiza Rais, ni vyema TAMISEMI ikatekeleza na kuwarejesha wagombea wa upinzani badala ya kuendeleza figisu ambazo hazina msingi. Demokrasi iachwe ichukue mkondo wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# *Wavulana nao wanastahili kulindwa, kuna shida kwao!*

Na Mwandishi Wetu

**KUMEKUWAPO** kampeni zinazoendelea kufanyika nchini kwa ajili ya kuwalinda watoto wa kike dhidi ya vitendo vya ukatili katika jamii.

Kampeni hizo zimekuwa zikiendeshwa na mashirika mbalimbali katika baadhi ya mikoa ambayo imeripotiwa kukithiri kwa vitendo hivyo.

Hayo ni mazito kuhusu ukatili kwa watoto na unyanyasaji wa kijinsia, hata kulifanya Jeshi la Polisi nchini kuanzisha Dawati la Jinsia katika vituo vyake ambako matukio hayo yamekuwa yakiripotiwa siri yanafanyiwa kazi.

Hapo kuna watuhumiwa kukamatwa na kuchukuliwa hatua, baada ya kufikishwa mahakamani na kupatikana na hatia.

Katika kampeni hizo, mara nyingi wazazi na walezi wamekuwa wakihimizwa kuwalinda watoto wa kike dhidi ya vitendo viovu, ikiwamo ubakaji na ndoa za utotoni, ili kuhakikisha wanatimiza ndoto zao katika maisha yao ya baadaye.

Taasisi na mashirika yakiwamo yasiyokuwa ya serikali nchini, yamekuwa yakijikita kuelekeza nguvu kwa ajili ya kuhakikisha watoto wa kike wanalindwa dhidi ya vitendo hivyo na vingine vya kutumikishwa katika ajira za majumbani wakiwa na umri mdogo hasa maeneo ya mijini.

> **Mashirika hayo yamekuwa wakifanya hivyo, kwa kuanzisha kampeni mbalimbali nchini kwa lengo la kumnusuru mtoto huyo wa kike na kutokomeza ukatili wa kijinsia kwao na wanawake.**

Mashirika hayo yamekuwa wakifanya hivyo, kwa kuanzisha kampeni mbalimbali nchini kwa lengo la kumnusuru mtoto huyo wa kike na kutokomeza ukatili wa kijinsia kwao na wanawake.

Kwa upande wa watoto wa kiume, imekuwa ni kidogo ukilinganisha na wa kike, kusikika kampeni hizo zikiwahusisha na kama matukio yapo ni machache, kama ya ulawiti.

Hivi karibuni, Jeshi la Magereza Nchini limenukuliwa likiwataka wazazi kubadilika mwelekeo wa malezi kwa kuelekeza nguvu kubwa kuwalinda watoto wa kiume na vitendo viovu katika jamii na kuwawezesha kuwa kina baba shupavu katika siku zijazo.

Kamishna wa Magereza anayesimamia Kamisheni ya Sheria na Uendeshaji, Nicodemus Tenga, alikaririwa akitoa wito huo kwenye Mahafali ya 64 ya Shule ya Sekondari Mzumbe ya wavulana wenye vipaji, iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.

Alitoa wito huo wakati akimwakilisha Kamishna Jenerali wa Magereza nchini, Jeremiah Katungu, katika mahafali hayo.

Wito huo sina shaka kuwa ni somo tosha kwa wazazi na walezi wa watoto hao nchini kuelekeza mwelekeo, pia kwa wavulana, kwani wao ni muhimu kwa ustawi wa familia zao kwa siku za usoni.

Akawaisitizaa wazazi wamuelewe anachokizungumza na kuweketa nguvu zao zaidi kuwalinda watoto wao wa kiume, kwa kuwa nao wapo katika hatari kubwa.

Hiyo ni kwa sababu wao waliopo katika vyombo hivyo ni mashuhuda kwa kile wanachokishuhudia.

Ingawa hakutaja hatari hizo, mara kadhaa watoto wa kiume wamekuwa wakidaiwa kuhushishwa katika matukio ya kutisha na mzazi, mlezi anakuja kugundua wakati akiwa mhalifu sugu, kushikiriwa na vyombo vya dola.

Ni sahihi alichokisema kwani jitihada zimeonekana zikifanyika katika jamii kuendelea kufanya kampeni zaidi ya kuwalinda watoto wa kike huku wakiume wakisahaurika.

Wakati umefika sasa kwa wazazi na walezi kuwalinda watoto wakiume ili waje kuwa bora zaidi katika ustawi wa familia zao na taifa kwa jumla.

Wazazi na walezi watafanikisha hilo kwa kutimiza wajibu wao kutengeneza familia imara.

Vilevile wazazi na walezi waelewe kuwa wao ni mtaji kwa kuzalisha watoto imara kwa manufaa ya kizazi cha kesho imara.

Tupaswa kuelewa kwamba, taifa lijalo la kesho litakuwa imara na salama endapo tukizingatia ushauri unaotolewa kwa wazazi na walezi kwa ajili ya makuzi ya watoto hao wa kiume.

# Dk. Mpango: COP29 iyape hadhi matumizi safi nishati ya kupikia

**BAKU, Azerbaijan**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ametoa wito kwa Mkutano wa COP29 kulipa hadhi ya kipekee suala la matumizi ya nishati safi ya kupikia katika mjadala wa kuhamasisha upatikanaji fedha za kudhibiti mabadiliko ya tabianchi.

Alitoa rai hiyo juzi ana wakati akihutubia Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) unaofanyika katika Mji wa Baku, Azerbaijan. Alisema takriban watu milioni 900 barani Afrika bado wanatumia nishati chafu katika kupika, hivyo kusababisha ukataji miti, upotevu wa sinki za kaboni na vifo kutokana na magonjwa yanayohusiana na moshi.

Makamu wa Rais alisema kuwa kutokana na umuhimu wa suala hilo, Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa kinara wa nishati safi barani Afrika. Hadi sasa tayari amezindua programu ya nishati safi ya kupikia ya kuwasaidia wanawake barani Afrika (Pan-African Women Clean Support Programme) inayodhamiria kuhakikisha nishati safi ya kupikia inatumika kama suluhu barani, inayogharimu takriban dola bilioni nne kwa mwaka hadi kufikia 2030.

Alisema hivi sasa Tanzania inatekeleza mkakati utakaohakikisha upatikanaji wa nishati safi, salama na nafuu ya kupikia kwa asilimia 80 ya kaya zote ifikapo 2034.

Makamu wa Rais alisema Mkutano wa COP29 unapaswa kuhakikisha ahadi za fedha zilizotolewa zinatekelezwa kwa kufanya maamuzi ambayo yatasaidia upatikanaji wa fedha kwa nchi kulingana na udharura na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Makamu wa Rais alisema bado masoko ya biashara ya kaboni hayajaainishwa vyema ikiwa ni pamoja na ukosefu wa taarifa zinazowezesha kushiriki kwa manufaa katika biashara hiyo, hali inayosababisha nchi kukosa malipo yanayostahili.

Alisema Tanzania imedhamiria kulinda na kuhifadhi bahari na misitu ambapo ina jumla ya eneo la hekta milioni 48.1 za hifadhi za misitu na makadirio ya uwezo wa kuhifadhi kaboni sawa na asilimia mbili ya jumla ya kaboni duniani. Vilevile, kuwapo ukanda wa pwani wa kilomita 1,424 na eneo la bahari la kilomita za mraba 64,500 ambayo inatoa fursa kubwa kwa uchumi wa buluu.



Dereva wa bajaji na muuza viazi wakiwa wameegesha vyombo vyao na kuziba njia ya waenda kwa miguu kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge, Dar es Salaam jana, kitendo kilichosababisha usumbufu kwa wapita njia. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wabunge waridhishwa utendaji PPPC

**Na Salome Kitomari**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeeleza kuridhishwa na kazi inayofanywa na Kituo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPC).

Aidha, kamati hiyo imeeleza kuharakisha mazungumzo na wawekezaji mbalimbali ili miradi 84 iliyo katika hatua mbalimbali ianze kutekelezwa.

Kamati hiyo ilisema hayo juzi wakati wa mafunzo kuhusu shughuli mbalimbali za kituo kwa lengo la kuwajengea uelewa wa miradi mbalimbali ambayo imeitambua kama muhimu kwa uwekezaji kitaifa hadi serikali za mitaa.

Mjumbe wa kamati hiyo na Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, alisema uamuzi unachukua muda mrefu kwenye mazungumzo, hivyo ni muhimu PPPC ikatathmini maeneo yenye urasimu na kuandaa mkakati, ikiwamo kuwa na eneo moja la kukusanya miradi ili kupunguza hali hiyo Pamoja na kuwa na maonyesho ya kutangaza kazi ili kupata wawekezaji.

> **"Kwenye ofisi yako (PPPC) ainisha maeneo yenye urasimu kama hizi sheria za ununuzi, ushindani ili viondolewe nae kazi iende kwa kasi, ikiwamo vivutio vya kikodi. Vitu vyote hivi vikusanye**

"Kwenye ofisi yako (PPPC) ainisha maeneo yenye urasimu kama hizi sheria za ununuzi, ushindani ili viondolewe nae kazi iende kwa kasi, ikiwamo vivutio vya kikodi. Vitu vyote hivi vikusanye wasilisha kwetu wabunge na upeleke serikalini ili viondolewe.

"Ukitengeneza mazingira mazuri utapata wawekezaji humu ndani, wenzetu Kenya wamepata wawekezaji kwenye barabara na wanakusanya fedha, tukishapata wawekezaji maana yake miradi yetu ya barabara itakamilika na tutakusanya fedha," alisema.

Pia alisema utayari wa Rais Samia Suluhu Hassan kwenye PPP ni mkubwa na kwamba ni muhimu wakaharakisha miradi mingi itoke kwenye makaratasi kwenda kwenye utekelezaji na matokeo kuonekana, na kwamba itawezekana ikiwa kwenye kila halmashauri wanakuwa na mtu maalum kwa ajili ya PPP.


"Mfano kuna timu za mipira zinaendeshwa na halmashauri, zinatakiwa zipate wawekezaji zitoke zisimamiwe taifa tutaona tija, tofauti na sasa zinavyoendeshwa zinatia hasara. Tuweke utaratibu mzuri wa kukusanya miradi halmashauri ikiwamo kuondoa urasimu wa mamlaka kukizana," alisema.

Mjumbe wa Kamati hiyo ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Salome Makamba, alisema awali alikuwa anachanganya kati ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na PPPC lakini namna walivyojipambanua kwa nguvu kubwa na matokeo yanaonekana, inatoa uhalali wa PPP kuendelea kuwapo.

"Namtia moyo David Kafulila (Mkurugenzi Mkuu wa PPPC) kazi anayofanya inaonekana na matunda tunayaona. Wabunge tunachotaka ni tija kwa nchi yetu. Lakini bado naona tuna miradi ya kimkakati ikiwamo wa gesi asilia ambao una zaidi ya miaka 11 na kila tukiuliza serikalini wanajibu mazungumzo yanaendelea, mmezungumza hadi mradi umepitwa na wakati kiasi kwamba tukienda sokoni sasa thamani ya gesi si ile ya wakati ule," alisema.

Awali, Kafulila alisema safari ya PPPC ilianza mwaka 2009 kwa kutungwa sera na baadaye sheria mwaka 2010 na kutungwa kanuni mwaka 2011 kwa ajili ya utekelezaji.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Wasisitiza uwekezaji TEHAMA elimu bora

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa elimu wamesema kuna umuhimu kwa nchi za Afrika, Tanzania ikiwamo, kuwekeza katika mifumo thabiti yenye uhakika wa upatikanaji wa elimu bora kwa wote katika nyakati zote hususani Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Wadau hao kutoka nchi za Afrika walisema hayo wakati wa Kongamano la Nne la Kimataifa la Elimu Bora (IQEC) linalofanyika jijini Dar es Salaam kwa siku tatu.

Akizungumza katika ufunguzi wa kongamano hilo, Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Faraja Nyalandu, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwekeza katika TEHAMA ili kuunganisha shule kwenye mtandao na kuwezesha utoaji wa elimu bora.

Faraja alisema kuwekeza nguvu kwenye eneo hilo kutasaidia pia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na kutoa wahitimu wenye uwezo katika sekta mbalimbali.

"Mlipuko wa UVIKO - 19 ulionesha hitaji la mifumo ya elimu ambayo inaruhusu watoto kujifunza, wawe ndani au nje ya darasa. Ni lazima tuhakikishe mazingira ya kujifunzia yanafaa hata wakati wanafunzi hawawezi kuhudhuria darasani moja kwa moja," alisema.

Pia alibainisha kuwa licha ya maendeleo katika sekta ya elimu, watoto wengi bado hawajaenda shule kutokana na changamoto mbalimbali.

Elke Wisch, mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Tanzania, alisema kuna haja kubwa ya uwekezaji katika elimu bora ili kukidhi mahitaji ya mabadiliko ya uchumi wa kidijitali na athari zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Katika muktadha huo, mabadiliko ya kidijitali si tu yanaongeza ufikiaji wa teknolojia lakini pia yanaimarisha uwezo wa mfumo wa elimu unaokuza zaidi ujuzi wa kidijitali kwa watoto wote katika karne hii ya 21," alisema Wisch.

Mmoja wa wanafunzi aliyeshiriki katika kongamano hilo, Hellen Anthony, aliishauri serikali na wadau kuongeza juhudi za kupambana na ukatili dhidi ya watoto.

Alisema watoto wengi bado wanakabiliwa na unyanyasaji na wako katika mazingira yasiyo salama.

Katika hotuba yake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema dhamira ya serikali ni kuboresha mifumo ya elimu na kuongeza bajeti katika sekta hiyo ya elimu.

"Kaulimbiu ya mkutano huu inatukumbusha wajibu wetu wa kujenga mifumo ambayo ni imara na endelevu, serikali tutaendelea kuhakikisha hilo linaimarishwa zaidi," alisema Mchengerwa.

Mchengerwa alisema mabadiliko yaliyofanywa kwenye Sera ya Elimu yana lengo zaidi katika kukuza fikra na stadi za wanafunzi kwa vitendo.




Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano wa tano wa maendeleo ya biashara na uchumi unaotarajiwa kufunguliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mkoani Dodoma. Wengine ni wasaidizi wake. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wataka sheria kuwarudisha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa elimu wamesisitiza utaratibu wa kuwarudisha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali uwe kisheria ili utekelezaji wake uwe endelevu.

Wameonyesha wasiwasi wao juu ya uendelevu wa suala hilo kwani kwa miaka ya nyuma lilikuwapo lakini alivyoingia rais wa awamu ya nne, Hayati John Magufuli aliliondoa na rais wa awamu ya tano,Samia Suluhu Hassan akalirudisha na kulitengenezea sera.

Waliyasema hayo juzi katika siku ya kwanza ya Mkutano wa Nne wa Kimataifa wa Ubora wa Elimu uliofanyika katika ukumbi wa kimataifa wa mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali.

Mkurugenzi wa Miradi na Ushirikiano wa Shirika la CAMFED, Anna Sawaki, alisema ni muhimu kwa utaratibu huo kuwa endelevu ili kuwanufaisha wanafunzi wengi watakaopitia changamoto za kimaisha.

Alisema kuna sababu mbalimbali zinazochangia wanafunzi kukosa masomo ikiwamo mimba za utotoni, utoro, mazingira magumu ya nyumbani, kutembea umbali mrefu hivyo mfumo huo unapaswa kuwa endelevu ili hata vizazi vijavyo vinufaike navyo.

Alisema licha ya serikali kuweka Sera ya Elimu na Mafunzo toleo la 2023 inayotoa fursa ya wanafunzi walioacha masomo kwa sababu mbalimbali kurejea shule kwenye mfumo rasmi na kukamilisha mzunguko wa masomo, kama isipokuwa endelevu haitosaidia watoto hao.

Alisema CAMFED inatekeleza sera hiyo kwa kuhakikisha kuwa inawasaidia wanafunzi waliohatarini kukatisha masomo kwa sababu mbalimbali kwa kuwapa misaada kulingana na changamoto zao kama vile pesa na vifaa na wale waliokatisha masomo kuwafanyia utaratibu wa kurudi shule au kujiendeleza kielimu.

Aliipongeza pia Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kuweka mifumo ya kutambua viashiria vya awali vya wanafunzi ambao wapo katika mazingira hatarishi ya kuacha shule na kuvitatua kabla tatizo halijawa kubwa.

"Na sisi tunaielimisha jamii juu ya viashiria hivyo ikiwamo walimu na wazazi ili pale wanapoona mwanafunzi ana dalili za kukatisha masomo waone namna ya kumsaidia na tunapohitajika tunatoa msaada, " alisema.

Alisema kupitia mradi huo wamewawezesha wanafunzi 711,726 kuendelea na masomo ikiwamo katika ngazi ya shule ya msingi, sekondari na mafunzo mbalimbali ili kujikwamua kiuchumi.Mratibu wa Mtandao wa Elimu (TEN/MED), Martha Makala, alisema kwa sasa nchi imepiga hatua kubwa kielimu kwa kuweka mpango huo katika sera ni matumaini yake kuwa suala hilo litakwenda kuwa kisheria ili utekelezaji wake uwe endelevu na kuwasaidia wanafunzi walioacha shule kurejea na kumaliza mzunguko wao.

Alisema mtandao huo kwa kushirikiana na taasisi nyingine zilizochaguliwa na wizara kuunda kamati ya kupitia sera ya elimu ya mwaka 1978 pamoja na maboresho mengine wamepeleka mapendekezo ya sera hiyo kuwapo katika sheria na ni matumaini yake kuwa ushauri huo utafanyiwa kazi.

"litakuwa na miongozo yake, litakuwa na sheria yake na kanuni zake, itatusaidia kama nchi kuhakikisha uendelevu wa watoto walioacha masomo kwa sababu mbalimbali na wao watapata haki yao ya masingi," alisema.

Makala alisema mtandao huo unaisaidia serikali kutekeleza elimu jumuishi kwa kutoa elimu kwa jamii ikiwamo wanafunzi waliacha masomo ili kurejea shuleni na kukamilisha mzunguko wao wa masomo.

"Tunajenga uelewa kwa jamii nzima kuhusu umuhimu wa wanafunzi wa kike na wakiume na wenye ulemavu kupata masomo kwa sababu ni haki yao ya msingi na ya kikatiba," alisema

Mkuu wa Idara ya Teknolojia ya Habari katika taasisi ya Jenga Huh, Maron Kakoti alisema kuwapo na sheria itakayosimamia mfumo huo utawapa nguvu asasi za kiraia kusaidia watoto kutoka katika makundi mbalimbali kupata elimu bila kuangalia tofauti zao.

Akifungua mkutano huo, Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa,amezitaka asasi za kiraia kuendelea kushiriki kikamilifu kuikumbusha serikali kutekeleza wajibu wake katika kuiboresha sekta hiyo.

Alisema asasi hizo zinamchango mkubwa katika kuisaidia serikali kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta hiyo ili kuleta matokeo chanya katika jamii kupitia elimu bora.

## Programu CBE yasajili biashara 412 nchini

**Na Joseph Mwendapole**

PROGRAMU atamizi ya biashara iliyoanzishwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), imefanikiwa kusajili mawazo 412 ya biashara ya wanafunzi wa chuo hicho ambayo yanaatamiwa ili yatoe matokeo makubwa.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, alisema hayo mwishoni wakati wa mahafali ya 59 ya chuo hicho yaliyohusisha wahitimu 2,665 wa ngazi mbalimbali.

Alisema program atamizi ya biashara ilianzishwa mwaka 2021 kwa lengo la kuwapa mafunzo ya biashara kwa vitendo wanafunzi hao wakiwa chuoni ambapo wanafunzi wamekuwa wakisajili bunifu zao za biashara na chuo kuwaendeleza wanafunzi hao wakiwa hapo hapo chuoni.

"Programu atamizi imekuwa na matokeo mazuri sana kwani wanafunzi wetu wengi wameanzisha biashara mbalimbali ambazo zimesimama na wakati wa convocation walifanya maonyesho ya bidhaa ambazo wanatengeneza," alisema.

Prof. Lwoga alisema katika kuwapa ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira chuo kilianzisha pia program ya uanagenzi ambayo inawawezesha kusoma nadharia na kufanya kwa vitendo.

Alisema kwenye program hiyo wameingia makubaliano na baadhi ya waajiri ambao huwapokea wanafunzi wa chuo hicho kufanya kazi huku wakiwa wanaendelea na masomo yao. "Programu ya uanagenzi ni kwamba mwanafunzi anasoma nusu ya muda wake darasani na nusu anakuwa kwa mwajiri na lengo ni kuhakikisha anapohitimu anakuwa na ujuzi wa kutosha unaohitajika kwenye soko la ajira," alisema.

Prof. Lwoga alisema hivi karibuni walianzisha kozi katika fani za ujasiriamali, uvumbuzi, uchumi, fedha, usafirishaji, usimamizi wa vifaa na masoko kidigitali zinazokwenda na soko la ajira. Alisema kozi hizo ni matokeo ya tafiti za kina na jitihada za muda mrefu zilizofanywa na timu yetu ya wahadhiri pamoja na wadau mbalimbali waliobobea katika tasnia husika.

Alisema kozi hizo zimezingatia mabadiliko ya teknolojia inayokua kwa kasi, mazingira ya uwekezaji, viwanda na biashara, na mahitaji ya soko la ajira.

Alisema kozi hizo zinakusudia kutoa ujuzi wa vitendo, maarifa ya hali ya juu, na mafunzo ya kina kwa wanafunzi wa chuo hicho ili kuwawezesha kufanikiwa katika soko la ajira na kukabiliana na changamoto za wakati huu.



# TAKUKURU yarejesha mamilioni mikopo ya asilimia 10 Same

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kilimanjaro imerejesha fedha za umma zaidi ya Sh. milioni 22.691 kutoka wanufaika wa vikundi vya mikopo ya asilimia 10 wa Kata za Stesheni, Same na Kisima za Halmashauri ya Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro.

Fedha hizo zilizorejeshwa ni kati ya Sh. milioni 548 zilizotolewa kwa wanufaika wa mikopo hiyo. Naibu Mkuu wa TAKUKURU Kilimanjaro, Saba Salehe, alisema kurejeshwa kwa fedha hizo ni matokeo ya ufuatiliaji wa miradi katika ripoti ya robo ya kwanza ya mwaka 2024/25.

"Tumefanya uchambuzi wa mifumo minane ili kubaini mianya ya rushwa na kuweka mkakati wa kudhibiti. Katika mifumo ya serikali tumechunguza mfumo wa marejesho ya fedha za mikopo iliyotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Same," alisema.


**serikali tumechunguza mfumo wa marejesho ya fedha za mikopo iliyotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Same," alisema.**

Julai 1, mwaka huu, serikali ilianza kutoa tena fedha za mikopo ya asilimia 10 kwa halmashauri nchini baada ya kusitishwa Bungeni, jijini Dodoma Aprili 13 mwaka jana.

Aprili 16, mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, alitangaza kurejeshwa kwa mikopo hiyo wakati akiwasilisha bajeti yake ya mwaka huu wa fedha wa 2024/25.

Mchengerwa, alisema halmashauri 10 za majaribio, zitaanza utoaji wa mikopo hiyo kwa kutumia benki.

Halmashauri zilizoteuliwa ni pamoja na ya Jiji la Dar es Salaam na Dodoma, Manispaa za Kigoma Ujiji na Songea (Ruvuma), Miji ya Newala (Mtwara) na Mbulu (Manyara), Wilaya za Siha (Kilimanjaro), Nkasi (Rukwa), Itilima (Simiyu) na Bumbuli (Tanga).




Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, Yosepha Komba (kushoto), akizungumza na wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa vijiji na vitongoji pamoja na wajumbe wa chama hicho, Kata ya Genge juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wapinga kutozwa 2,000/- kukarabati barabara

**Na Godfrey Mushi,** ARUMERU

WAMILIKI wa magari na pikipiki wamepinga kutozwa Sh. 2,000 kila Jumamosi kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya Barabara ya Oldonyowasi Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha kwa ajili ya kupeleka mazao na wafanyabiashara mnadani

Wamiliki wa vyombo hivyo vya usafiri, akiwamo Loshie Laizer, Mkazi wa Kisimiri Juu, waliliambia Nipashe kuwa wanapinga kutozwa kiasi hicho kila mmoja kwa kuwa wakati mwingine hawafanyi kazi.

"Ni lazima utoe ili uweze kupita. Hakuna risiti (stakabadhi) unayopewa, zaidi unaandikwa namba na aina ya pikipiki na kama ni gari hivyo hivyo.

Ukiuliza ni ya nini unajibiwa fedha hizo ni kwa ajili ya ukarabati wa barabara," alisema Laizer.

Jumamosi ni siku ya mnada katika Kata ya Oldonyowasi ambayo uongozi wa mtaa huo umelenga kukusanya fedha hizo ili kupata mapato mengi kulingana na idadi ya watu wanaofika sokoni hapo mnadani. Mkazi wa Losinoni, Kiring'a Telele alisema kuwa: "Uchumi mkubwa tunaotegemea huku ni mahindi, maharage tupeleke sokoni kwa usafiri, tuuze."

"Tuangalie sasa bei ya debe la mahindi, labda mahindi yakienda sana kwa debe ni 7,000. Ukodi bodaboda akupeleke wewe na debe moja, ufike tena hapo ulipe shilingi 2,000 za barabara. Mwananchi hapo anakuwa kwa ujumla amepata hasara,"aliongeza Telele.

Alipoulizwa mmoja wa wakusanya fedha hizo, Julius Mollel, Mkazi wa Kijiji cha Losinoni, alisema kiasi hicho wanachozwa kwa upande wake ni cha kawaida kwa sababu wakati wa mvua, barabara yao haipitiki kirahisi.

"Kwa hiyo sisi tunaona ni jambo la kawaida kwa sababu tukikusanya hiyo pesa tunaweka moramu au kokoto sehemu korofi kama hapo mbele na hapo nyuma. Hayo maeneo huchimbika wakati wa kiangazi na wakati wa mvua, magari hayapiti yanateleza.

Ili kupata ufumbuzi wa jambo hili, Mbunge, Serikali ngazi ya Kata na halmashauri au TARURA, wanapaswa kuja hapa na kuona ukubwa wa tatizo na kulitafutia ufumbuzi wa haraka ili tuachane na haya mambo ya kutoza wananchi 2,000 kulipia barabara.

Zaidi aliongeza: "Wananchi wanaotumia hii barabra ni zaidi ya 3,000. Wananchi wa Kijiji cha Losinoni Kati, Oldonyowasi, Kisimiri nao wanalipa kwa sababu wakati tunatoa maji kwenye barabara wao hawapo."

Alisema wanaotozwa kiasi hicho ni dereva wa gari au wa pikipiki na sio abiria.

Diwani wa Oldonyowasi, Kijana Mollel, akizungumzia sakata hilo, alisema anaamini hayo ni makubaliano baina yao na uongozi wa kijiji.

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko hayo, Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Arumeru, Julius Kaaya alisema hana taarifa na kusisitiza kuwa hicho ni kikundi cha wezi wanaojipatia fedha kwa njia ya udanganyifu

"Hatujui kitu kama hicho, wala hakipo kabisa, hao ni wezi tu kama wezi wengine. Tunatenga fedha za matengenezo ya kawaida ya barabara hiyo kila wakati.

# Wachimbaji Tanzanite watakiwa kuchangia maendeleo

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

KAMPUNI za uchimbaji madini ya Tanzanite katika Wilaya ya Simanjiro mkoani hapa zimetakiwa kusaidia ujenzi wa mabweni ya wanafunzi na zahanati katika maeneo yanayowazunguka ili kunufaisha jamii .

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Gracian Makota,

alitoa rai hiyo wakati akizungumza na wadau wa madini hayo katika mji wa Mirerani,

Makota alizitaka kampuni hizo kuiga mfano wa kampuni moja kwa kutoa misaada kwa jamii katika wilaya hiyo ikiwemo ya ujenzi wa mabweni na zahanati kwa manufaa ya wananchi.

Alisema hivi karibuni kampuni hiyo imechangia Sh.milioni 20 kwenye Zahanati ya Kijiji cha Naepo na Sh. milioni 60 miradi ya elimu Mji Mdogo wa Mirerani na Kata ya Naisinyai.

"Unapotoa misaada kwa jamii (CSR) ishirikishe Serikali, tutatoa na cheti na siyo kusaidia mtu mmoja kwani jamii haitanufaika ni kama umeenda kwenye dansi ukatajwa jina papaa fulani ukagawa fedha kwa waimbaji," alisema.

Alisema halmashauri hiyo, imepanga kutekeleza miradi 18 yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 1 kupitia fedha za wadau wa madini ya Tanzanite kuwajibika kwa jamii.

Makota, alisema miradi hiyo itajengwa kwenye kata tofauti kwa lengo la jamii ya Simanjiro kunufaika kupitia rasilimali inayowazunguka ya madini hayo.

Ofisa Madini Mkazi (RMO) Mirerani, Nchagwa Chacha Marwa, alisema uchangiaji maendeleo kwa jamii ni takwa la kisheria, hivyo wachimbaji madini watekeleze.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Baraka Kanunga aliwashukuru wadau wa madini waliohudhuria kikao hicho kwa anaamini watapokea maoni yao kwa kutekeleza miradi hiyo.

Mchimbaji wa madini hayo, Eliaman Mgala, alisema elimu ya kuchangia miradi hiyo inapaswa kuendelea kutolewa kwao kwa manufaa ya jamii ya wilaya hiyo.

"Hata kwenye nyumba za ibada kuna sadaka zinatolewa, hivyo wachimbaji tunapaswa kuelezewa zaidi ili tuweze kushiriki kuchangia miradi ya maendeleo katika wilaya hii ya Simanjiro," alisema Mgala.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA) Tawi la Mirerani, Peter Loiting'id Laizer, alisema baadhi ya wachimbaji wanachangia maendeleo, lakini kwa upande wa serikali hawatambuliki.

"Wachimbajia wengine huwa wanaombwa misaad ya maendeleo na jamii inayowazunguka ila hawatambuliki kwa sababu hawatoi taarifa serikalini," alisema Laizer.





## Wagombea CHADEMA waliokatwa wamwangukia Samia

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

BAADHI ya wagombea kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Manispaa ya Shinyanga ambao majina yao yameenguliwa kushirika katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wamemuomba Rais Samia Suluhu Hassan, alitafakari jambo hilo na kuingilia kati.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wakizungumza na vyombo vya habari, kwenye Ofisi za CHADEMA Kanda ya Serengeti iliyopo Manispaa ya Shinyanga.

Mmoja wa wagombea hao, John Emmanuel, alisema jambo la wagombea wa upinzani kuondolewa majina yao ni aibu kwa taifa, kwamba Rais Samia anapaswa kutafakari jambo hilo kwani linavuruga uchaguzi.

"Uonevu huu wa kuondolewa majina unasababisha taifa kwenda kwenye machafuko ya kisiasa, tunamuomba Rais Samia alitafakari jambo hili, wagombea wote warudishwe majina yao ili tupambane majukwaani," alisema Mkasha.

Alisema yeye ameondolewa jina lake akidaiwa kujaza umri tofauti na uliopo katika daftari la wapiga kura, kudai kuwa ni uongo kwani taarifa zake alizijaza kwa usahihi.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Serengeti, Jackson Mnyawami, alisema zaidi ya asilimia 95 ya wagombea wao wameondolewa kwa sababu mbalimbali ambazo zipo nje ya Kanuni ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024, huku wengine wakiwekewa pingamizi batili ikiwemo kuwa mgombea ana wake wengi.

Hivyo, alimuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa na wasimamizi wa uchaguzi kutenda haki katika rufani watakazoziwasilisha dhidi ya wagombea wao na kurudisha majina ya wagombea wote.

Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Shinyanga, Sebastian Polepole, alisema hali hiyo inawanyima haki ya kikatiba wananchi kupiga kura na kuwachagua viongozi ambao wanawataka.

Msimamizi wa Uchaguzi Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, alisema hakuna mgombea wa CHADEMA ambaye ameondolewa kimakosa, bali wamejiondoa wenyewe kwa kutokidhi vigezo.

Alisema baadhi ya wagombea walikosea kujaza majina kwenye fomu na kwamba mfano mtu ni wajinsia ya kiume lakini amejaza kwenye jinsia ya kike, huku wengine wakiwa hawaja jiandikisha kwenye Daftari la Makazi la Mpiga Kura, pamoja na kujidhamini wenyewe badala ya chama.

Alisema kwa mgombea ambaye hajaridhika na uteuzi huo wa majina anayo haki ya kukata rufani na kupeleka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Rufani, ambaye ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, Said Kitinga.

# Wagonjwa wakosa huduma kisa mifumo

Na Shaban Njia, KAHAMA

MIFUMO ya ukusanyaji wa mapato katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imetajwa kusababisha wagonjwa hasa wajawazito na watoto kukosa huduma ya matibabu kwa wakati.

Chanzo cha hali hiyo ni kutokana na mifumo hiyo kuchukua muda mrefu kupokea malipo na kusababisha wagonjwa kukosa huduma ya haraka.

Hayo yamebainishwa juzi na madiwani wa halmashauri hiyo katika kikao cha kawaida cha robo ya pili ya mwaka 2024/25 na kueleza kuwa wagonjwa wamekuwa wakikosa matibabu kwa wakati pale kunapotokea tatizo la mfumo ya ukusanyaji wa mapato. Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Kahama Mjini, Mkora Kabale alisema, wagonjwa wanaofika katika hospitali hiyo wamekuwa wakikosa matibabu kutokana na mfumo ya ukusanyaji wa mapato inapoleta shida. Hivyo, aliiomba serikali kutumia njia mbadala ili waweze kulipia na kupata matibabu kwa wakati.

> **"Tunafahamu mifumo yetu hospitalini inatusaidia kukusanya mapato na hakuna upotevu wowote wa fedha, lakini inapoleta shida au kuwa na tatizo inasababisha wag-**

"Tunafahamu mifumo yetu hospitalini inatusaidia kukusanya mapato na hakuna upotevu wowote wa fedha, lakini inapoleta shida au kuwa na tatizo inasababisha wagonjwa wetu wanaofika kupata matibabu hasa wajawazito na watoto kukosa huduma, hivyo tunaomba kutafuta njia mbadala ya tatizo hili," alisema Kabale.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Masudi Kibetu akijibu hoja hiyo alikiri kuwepo kwa tatizo la mfumo linalosababisha kuwepo kwa changamoto ya utoaji wa huduma kwa wagonjwa wanaofika hospitali kupata matibabu na kueleza kuwa wameweza kulishughulikia tangu Septemba mwaka huu.

Alisema kila wanapopata taarifa za mfumo kuleta shida amekuwa akituma Ofisa Tehama ili kwenda kuhakikisha na kuangalia namna sahihi ya kuendelea kutoa huduma, huku wakiendelea kuangalia njia sahihi ya kurekebisha. Alisema mifumo imesaidia kuongeza mapato kutoka Sh.milioni tatu kwa siku mpaka kufikia Sh.milioni nane.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Phabiani Kamoga alipongeza manispaa kwa kuendelea kusimamia mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kuwataka kuendelea kubawana watumishi ili kutokaa na fedha mkono na badala yake wazipeleke benki kwa wakati.




Wanafunzi wa Sekondari ya Bigwa, mkoa wa Morogoro wakiwa na zawadi zao baada ya kushika nafasi ya kwanza kwa kipengele cha uwasilishaji wa mada ya mashine za kielektroniki, katika shindano la vilabu vya kodi, kwa shule za sekondari linaloendeshwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), shuleni hapo, mkoani humo, juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Uraia wamkwamisha diwani 'mstaafu' kugombea

Na Ambrose Wantaigwa, TARIME

ALIYEWAHI kuwa Diwani wa Kata ya Sirari, Tarime mkoani Mara kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Nyangoko Paulo ameenguliwa katika kinyang'anyiro cha nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Mpakani kwa madai kuwa siyo raia wa Tanzania.

Kwa mujibu wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika kijiji hicho, Paulo anadaiwa kuwa na kitambulisho cha Kenya, hivyo kukosa sifa ya kuendelea katika mchakato baada ya kuwekewa pingamizi na mgombea mwenzake.

Akizungumza wakati akiwasilisha rufani ya kupinga kuenguliwa katika kijiji hicho kilicho jirani na Kenya, mgombea huyo alisema aliwahi kushika nafasi ya udiwani kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 na pia amewahi kuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho kwa zaidi ya miaka 10.

"Mimi nimewahi kushiriki uchaguzi miaka iliyopita kama mtanzania na nikichaguliwa katika vipindi na nafasi mbalimbali katika eneo hili nilipozaliwa. Lakini nashangaa mwaka huu nawekewa pingamizi na mgombea mwenzangu kuwa mimi siyo raia na limekubalika," alisema Paulo Mwenyekiti wa CHADEMA Jimbo la Tarime Vijijini, Mrimi Zablon, alisema wagombea 13 wa chama hicho nafasi za wenyeviti wa vijiji wameenguliwa kati ya vijiji vyote 88 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uraia na ulevi uliokithiri.

"Pia wagombea wetu 150 katika nafasi za vitongoji 500 jimbo zima wameenguliwa, kutokana na sababu ambazo baadhi hazina mashiko kulingana na mwongozo na sera za uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema.

Alisema sababu zilizo kinyume na utaratibu zilizotolewa na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ni pamoja na baadhi ya wagombea wa chama chao kudaiwa kuwa walevi pamoja na kugombanisha ndoa za wanajamii. "Kanuni za uchaguzi zimeainisha sifa za mgombea zinazoeleweka kama vile, umri, uadilifu katika utii wa sheria pamoja na uraia lakini sababu zilizowekwa na wenzetu hazina mashiko ya kuwezesha kuondolewa kuwakilisha katika nafasi hizo," alisema.

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Tarime, Mwita Isasi aliwataka wanachama wote kuwa watulivu wakati huu waratibu wa kisheria wakiwasilisha rufani katika Kamati ya Wilaya akiamini wagombea wao watarudishwa.

Alisema chama hicho kimejifunza kutokana na uchaguzi uliopita miaka ya nyuma kwamba mara nyingi vurugu za kisiasa zinaanzishwa na baadhi ya wasimamizi wasaidizi kushindwa kutenda haki kwa wagombea kutoka vyama vyote.

Alisema: "Hadi sasa amani ya majimbo yote mawili ya Wilaya ya Tarime Mjini na vijijini itategemea maamuzi ya kamati ya rufani ambayo ina weledi wa kutenda haki kwa kurudisha wagombea wetu wote washiriki zoezi hili ambalo ni haki yao kikatiba".

ama
ALHAMISI NOVEMBA 14, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**KUELEKEA UDHIBITI WAKE 2030..**

**Changamoto na mbinu za kumtaarifu mtoto VVU vyake, kutoka kwa mama**



Ukurasa 13

Mama mwenye UKIMWI, aliyeacha ARV kwa ushawishi wa maombezi




Ukurasa 14

**DK. SAMIA NA VITA UKIMWI**

**Kafikisha tiba 96% kusonga sifuri, 'mbishi' anayejitokeza unyanyapaa**

WATAALAMU AFYA WAELIMISHA:

# Ujue ugonjwa maburg usiotibika, umefafana na UKIMWI, tofauti...

**Na Pilly Kigome**

KUNA ugonjwa mpya sasa unaoitwa maburg, unaosababishwa na virusi vyenye jina hilo, ukiwa na sifa unaambukizwa kwa haraka sana.

Ni miongoni mwa magonjwa ya mlipuko yenye sifa za homa za virusi zinazosababisha kutokwa damu mwilini.

Hadi sasa Wizara ya Afya inatoa mafunzo kuelimisha umma, kuhusiana na magonjwa ya mlipuko aina hiyo, ikifahamisha jamii, moja ya makundi yanayopewa elimu ni waandishi wa habari, ikiaminika ni watoaji elimu kwa umma, kwa kuwa wao ni kioo cha jamii na wanafikisha ujumbe mbali.

Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Afya kwa Umma katika Idara ya Kinga, katika Wizara ya Afya, Dk. Ona Machangu, akielimisha wanahabari kuhusu ugonjwa huo, akiwapa mbinu na namna mbalimbali ya kujikinga na maambukizi yake, hali kadhalika kubainisha dalili zinavyopatikana ugonjwa huo na mengi.



Matabibu wakimhudumia mgonjwa anayesadikiwa na maradhi ya maburg. **PICHA: MTANDAO**

Dk. Machangu anaanza kwa kuelekeza namna ugonjwa huo unavyoenea na kuambukizwa, akibainisha unaenezwa haraka kutoka kwa mtu mwenye maambukizi hadi kwa mwingine, kupitia njia nyingi, ikiwamo kugusana ngozi.

Pia anataja hali ya kugusa maji ya mwili wa mgonjwa kama vile damu, mate, matapishi, kinyesi, machozi, kamasi, jasho au mkojo.

Vilevile anataja namna ya kugusa au kuosha maiti ya mtu aliyefariki akiwa na dalili za ugonjwa wa marburg, vyombo, nguo, matandiko au godoro la mwenye maambukizi ya virusi vya marburg.

Dk. Machangua anasema, suala la kuchangia vitu vyenye ncha kali na mwenye maambukizi ya ugonjwa huo, ikiwamo kujamiiana na mtu mwenye virusi vya marburg.

Mjamzito huyo anaelezwa kuwa na uwezo wa kumwambukiza mtoto wake maradhi hayo, ilhali bado yuko tumboni au wakati anapomnyonyesha, anaweza kupata maambukizi hayo.

Aidha, inatajwa maambukizi hayo yanaweza kutokea kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, iwapo mtu atakula au kugusa mzoga au wanyama wenye virusi vya ugonjwa huo, kama vile popo, tumbili, nyani au sokwe.

Aidha ugonjwa huo unathibitishwa kuambukiza kwa njia ya hewa, kama unavyodhaniwa na wengi.

**UNAFANANA NA UKIMWI**

Inatajwa kwamba, licha ya kutoambukizwa kwa njia ya hewa, ugonjwa huo huwa unatajwa wasifu wake unapoangaliwa kwa kina, unatajwa maambukizi yake yanashabihiana na Ugonjwa wa Ukosefu wa Kinga Mwilini (UKIMWI).

Hiyo inafafanuliwa kwamba, kuna baadhi ya aina ya maambukizi yanafanana na jinsi yanavyopatikana maambukizi hayo ya Ukimwi.

Eneo moja linalofanana linatajwa ni katika vitu vyenye ncha kali, kuosha maiti ya mwathirika, kujamiiana, hata suala la kunyonyesha mtoto.

Hapo ni pale mama anayeathirika humhamishia mtoto maambukizi, pale mama atakapokuwa hajaanza kutumia dawa ipasavyo.

Dk. Norman Jonas, Bingwa Mratibu Kitaifa wa Huduma za Afya ya Jamii, anawaambia wanahabari kuwa dalili zake huanza kuonekana kati ya siku mbili hadi 21, baada ya kupata maambukizi.

Anafafanua kuwa dalili hizo, ni pamoja na mwili kuishiwa nguvu, vidonda vya koo, vipele vya ngozi, maumivu ya tumbo, kutapika.

Vilevile ni katika eneo la kutokwa na damu katika sehemu za wazi kama vile puani na kwenye matundu mengine, kutapika, pia kuharisha damu.

**INAENDELEA UK.14**

AFYA

KUELEKEA UDHIBITI UKIMWI 2030...

# Changamoto na mbinu za kumtaarifu mtoto VVU vyake, kutoka kwa mama

**Na Beatrice Moses**

INAPOTAJWA suala la Virusi Vinavyosababisha Ukimwi (VVU), huwa vinaendana na kuwapo taarifa za aina mbalimbali, zikiwamo za mafanikio, sherehe, ugonjwa au msiba, zote zina njia zinazojulikana na zinapaswa kuzingatiwa kuhakikisha zinafika kwa wakati sahihi.

Ndipo kunatajwa kuwapo njia nyingi za kufikishaji taarifa za ugonjwa na mwongozo maalum wa taifa unaosimamiwa na Wizara ya Afya.

Pia serikali kwa kutambua umuhimu huo kwa mtoto walioambukizwa VVU, namna ya kumfanya atambue hali yake kutatua changamoto alizo nazo, zimekuwa zikiwakumba wazazi au walezi, sasa kumetolewa kutoa mwongozo maalum wa namna ya kufikisha taarifa kwa njia sahihi.

Dk. Lilian Mwakyosi, anayejihusisha na kuelimisha jamii kuhusu Ukimwi na HIV, anasema kuna umuhimu mtoto kupewa taarifa kama amepata maambukizi ya VVU, lakini unapaswa kuzingatia mwongozo wa nchi unaoelekeza namna nzuri ya kufikisha hizo taarifa taratibu, kulingana na umri wake.

"Mtoto asipoambiwa kuna athari zinazoweza kujitokeza, hawezi kuwa makini katika kunywa dawa kwa usahihi kwa kuwa hajui anakunywa kwa sababu gani.

"Pia, alikuwa anaweza kusababisha maambukizi bila ya kujijua baada ya kwenye uhusiano," anasema Dk. Lilian, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya DARE.



Dk. Lilian Mwakyosi, mtaalamu mwenye ufafanuzi. **PICHA: BEATRECE MOSES**

Katika mwongozo wa Wizara ya Afya, unaeleza mtoto anapofikisha umri miaka minne hadi sita, anatakiwa aanze kupewa taarifa kwa hatua kuhusu maambukizi yake.

Inafafanuliwa pale mtoto anapofikisha kati ya miaka nane hadi 10 na anaonekana ana uwezo wa kuelewa masuala ya maisha na anamudu masomo darasani, mtoto huyo atakuwa na uwezo kuelewa masuala ya afya yake na kinga inavyofanya kazi mwilini.

Inatarajiwa katika umri huo, atapewa taarifa kamili kuhusu hali yake ya maambukizi ya VVU. Pia, inabainisha umuhimu wa mzazi au mlezi, kwa kushirikiana na mtoa huduma, wakaandaa mpango kumweleza mtoto hali yake, kabla hajataarifiwa na vyanzo vingine.

"Kusikia habari kuhusu hali yake ya maambukizi kutoka kwa mtu mwingine, kunaweza kumfanya mtoto ajisikie vibaya na atingwe na msongo wa mawazo na hata kupeleka kuchukua maamuzi yasiyofaa kama vile kujiua, kuacha shule, kuacha dawa hata kutokuwa na imani na wazazi wake," inaelezwa.

Katika taarifa hiyo, inaelezwa mtoa huduma anatakiwa kuzingatia mambo kadhaa kabla ya kumweleza mtoto mwenye VVU hali yake.

Hapo kunatajwa hitaji la kutathmini uwezo wa mtoto kukabiliana na taarifa za kushtua, pia uwapo uhusiano mzuri kati ya mlezi au mzazi, mtoto, pia mtoa huduma.

**VVU VINAVYOMPATA MTOTO**

Kuna ufafanuzi wa wataalamu wa afya, kwamba anaweza kuambukizwa VVU kwa kuchangia mswaki na vitu vyenye ncha kali kama vile sindano na nyembe, kisha akaongezwa damu yenye VVU.

Kuna sehemu kwenye utumiaji dawa za kulevya kwa njia ya sindano unafanyika, watoto pia wanakuwa hatarini kupata maambukizi ya VVU, kwa kuchangia sindano husika.

Pia, inatajwa maambukizi kwa njia ya ngono hutokea kwa watoto wanaoanza wakiwa katika umri mdogo, kukiwapo maelezo:

"Baadhi ya sehemu kuna dhana potofu kwamba VVU inapona na kuisha kabisa pale unapofanya ngono na mtoto mdogo au mtoto ambaye hajawahi kufanya ngono. Hivyo kufanya watu wanaoishi na VVU kuwabaka watoto na kuwaambukiza VVU," inaelezwa.

Usafirishaji haramu watoto kwa visingizio vya kuwapatia elimu au kazi bora, nako kunatatajwa kuwaweka watoto hatarini kupata maambukizi ya VVU, kwa kulazimishwa kufanya biashara ya ngono na hata kubakwa.

**HATUA ZINAVYOCHUKULIWA**

Hapo kisaikolojia kunatajwa utayari wa mlezi au mzazi kumweleza mtoto wake mwenye VVU hali yake ya maambukizi, wajibu akiubeba mtoa huduma akishirikiana na mlezi au mzazi.

> **Pia, inatajwa maambukizi kwa njia ya ngono hutokea kwa watoto wanaoanza wakiwa katika umri mdogo.**

Ni hatua inayoanza na kuandaa mpango wa kumweleza mtoto hali yake ya maambukizi utakaokidhi mahitaji ya mtoto na familia husika, ikisisitizwa umuhimu wa kuwapo mawasiliano endelevu kuhusu afya ya mtoto, kwa kuwa mtoto anapozidi kukua,uelewa wake pia unapanuka.

Hivyo, inatajwa kuwa mtoa huduma anapaswa kuzungumza na mzazi au mlezi, faida na hasara za kumweleza mtoto mwenye VVU hali yake, wachukue kwa busara uamuzi wa pamoja.

"Kumbuka kumweleza mtoto mwenye VVU hali yake ya maambukizi hakuhitaji haraka. Pata muda wa kutosha wa kushauriana na mtoa huduma namna ya kutoa taarifa hiyo kwa mtoto wako," unaeleza kipeperushi cha mwongozo wa Wizara ya Afya.

Monika Jorum (siyo lake halisi), anaishi na VVU, akiwa na maelezo ya masikitiko kuwa alifiwa na mwanawe mwaka 2007 akiwa na umri wa miaka saba, lakini baada ya kifo ndiyo ikajulikana tayari naye alikuwa na VVU.

Anasema, alijifungua mwanawe akiwa na afya njema na hakufahamu wao kuwa na VVU. Baada ya miaka kadhaa, mwanawe alianza kuugua kifua, akatibiwa pasipo hali ya kutengemaa.

"Naamini ningekuwa nimejua mapema pengine ningemsaidia naye aweze kupata dawa. Pia, ningemweleza kwa kuwa ndugu zake nimeshawaeleza, japo wao hawana maambukizi ya VVU, lakini naamini kuwa taarifa ni muhimu kwao na kwangu pia," anasema Monika.

**KUTOKA TACAIDS**

Kaimu Meneja wa Mipango na Bajeti wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Renatus Mukasa, ana maelezo kwenye mafunzo maalum yaotawyo 'Science Cafe' yanayosimamiwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA).

Anasema, kuna haja ya elimu ya kuzuia maambukizi ya HIV kuendelea kutolewa kwa msisitizo, ili ama kukumbusha au kuongeza umakini wa mapambano.

Mukasa anadokeza kwa kutumia Utafiti wa Kitaifa wa Athari za VVU Tanzania 2022-2023 uliofanywa majumbani, uligundua kulikuwapo takriban mikasi mipya 60,000 za maambukizi ya VVU miongoni mwa watu wazima nchini.

INAENDELEA UK.13

AFYA

# Mama mwenye UKIMWI, aliyeacha ARV kwa ushawishi wa maombezi

## • Magumu aliyoanzia; leo asaka mume...

**Na Mwandishi Wetu**

NILIACHA Dawa za Kufubaza Virusi vya Ukimwi (VVU) maarufu ARV kutokana na ushawishi wa ndugu yangu mmoja aliyenipeleka kwenye maombi," Doreen Odemba, anayesimulia mkasa uliomkuta alipoenda kwenye maombi akiaminishwa angepona maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Anasema, alipofika kwenye maombi akaambiwa aache dawa, naye akatii, akifafanua aliacha kutumia dawa kwa muda na alipokwenda kupima afya, bado akakutwa kuwa na maambukizi hayo.

Doreen mwenye umri wa miaka 30 sasa, anasema baada ya hapo akapatwa na changamoto ya kiafya, alikumbwa na kiharusi kilichomsababisha kushindwa kujihudumia kwa takribani miaka miwili.

"Nilipata kiharusi, nikakonda sana nikawa wa kubebwa, hata ikafikia kujisaidia kwenye nepi kama mtoto,"anaeleza na kuongeza kuwa:

"Hii imenifundisha sana, sirudii kuacha dawa, niwasisitize wengine wenye hali kama yangu wasiache dawa kwa kuambiwa kwamba wameponywa."

### ALIVYOFAHAMU KAATHIRIKA

Doreen anaeleza simulizi yake kwa huzuni:"Nakumbuka dada aliyekuwa akifanya kazi za ndani nyumbani kwa mama mkubwa, alinitamkia kwa kunikaripia kutokana na utundu wangu wa kitoto. Hivi Doreen unajua kuwa wewe una Ukimwi?'

"Baada ya hapo, nilikwenda kumuuliza mama mkubwa ambaye alinijibu kuwa ni ukweli, ndiyo maana unakunywa dawa na kwamba nilizaliwa na maambukizi hayo.'

Doreen anasema alipofahamu hayo akiwa na umri wa miaka 12 na kisha kuanza kutumia dawa za kufubaza VVU mwaka 2004.

Japo haikuwa rahisi kwake kupokea kwa wepesi, Doreen anasema shuleni tayari ugonjwa huo ulikuwa ukifundishwa haikuwa vigumu kuelewa kuhusu kuwa na virusi vya Ukimwi, japo anadai ilimhuzunisha.

Doreen anasema lengo lake kubwa sasa, ni kuisaidia jamii kijumla kutokomeza unyanyapaa, kadhalika kuwapa matumaini wenye hali kama yake kwamba, kupata maambukizi si kufa.

"Baadhi ya watu kwenye jamii si waelewa kabisa, lakini ukiwa kwenye hali hii bado unaweza kuwa na ndoto vilevile kufurahia maisha,"anasema Doreen.

Anasema hata baada ya kuelezwa kuwa ana hali ile, baadhi ya watu walimtakia "amechoka kudanga ndo maana amejitangaza, wengine walisema ameumizwa na mapenzi si bure'.

Anasema baadhi ya ndugu walimnyanyapaa mwanzoni lakini sasa wengi wanamchukulia kawaida.

"Nakumbuka nilinyimwa fursa ya kupika chakula, baadhi ya watu waliokuwa wakifahamu kuhusu hali yangu walianza kusema pale kuwa nina virusi. Baada ya hapo nilinyimwa kazi ya upishi katika mgahawa mmoja jijini Dar es Salaam," anafafanua.

Hata hivyo, unyanyapaa haujamkatisha tamaa. Anasema hajachoka kulizungumzia kwenye mitandao ya kijamii ambako anafurahi kukutana na watu wengi wenye hali kama yake ambao kupitia yeye wameongeza kujiamini na kujithamini.


Mwanamama Doreen Odemba. **PICHA: MTANDAO**

### ANATAMANI KUOLEWA

Mama huyo anasema, suala la uhusiano kwake amelipa umuhimu sana, kwa kuwa anatamani kuolewa na mtu ambaye hana maambukizi.

Pia, anarejea uzoefu wake kimaisha, anasema wanaume wasio na maambukizi wanajali afya wanapokuwa katika uhusiano na wanawake wenye maambukizi.

"Unajua mimi nina maambukizi, halafu kusema ninataka kuolewa na mwanaume mwenye maambukizi kama mimi, naona hiyo ni kujinyanyapaa.

"Hivyo nitapenda yule asiyekuwa na maambukizi ili kupunguza kujinyanyapaa," anafafanua Doreen.

Mwanamke huyo kwa sasa akijishughulisha na ujasiriamali kumudu maisha yake, anasema unyanyapaa umezima ndoto za watu wengi wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi.

"Ninatamani kuona jamii ikishirikiana na serikali na taasisi nyingine za kiraia kutoa elimu sahihi ya VVU," anashauri.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Kimataifa la Kupambana na Ukimwi (UNAIDS), asilimia 44 ya maambukizi mapya ya VVU yanawaangukia wanawake na wasichana na kila wiki kuna wanawake, vijana na wasichana 4,000 duniani kote huambukizwa VVU na kati yao, 3,100 wapo nchi za Afrika zilizo Kusini mwa jangwa la Sahara, kunakopatikana Tanzania na Kenya, aliko Doreen.

***• Kwa mujibu wa BBC***

# Changamoto na mbinu za kumtaarifu mtoto VVU vyake

**INATOKA UK.12**

Mukasa ambaye ni Mchumi Mwandamizi, anaeleza utafiti umebaini kuwapo tofauti kubwa katika kiwango cha maambukizi ya VVU kulingana na umri, jinsia na kanda zilizopo.

"Kiwango cha juu cha maambukizi kilikuwa miongoni mwa wanawake na katika baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara. Kiwango cha maambukizi ya VVU kilikuwa chini ya asilimia moja katika mikoa yote ya Zanzibar," anasema.

Mukasa anaongeza kuwa, suala la kusonga mbele katika lengo la Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Ukimwi (UNAIDS) la mwaka 2030 la kumaliza Ukimwi, kunahitaji umakini wa ufuatiliaji unaoendelea kugundua maambukizi mapya yalivyo.

Pia anataja tiba kutolewa kwa wakati na huduma za kinga mchanganyiko za kuzuia maambukizi zaidi zikipatikana.

Katika utafiti huo, pia ulitoa taarifa muhimu kuhusu maendeleo ya kitaifa na kikanda kuelekea kudhibiti janga la VVU ikiwamo maendeleo kuelekea kufikia malengo ya 95-95-95 ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Kudhibiti Ukimwi (UNAIDS).

Tanzania hadi sasa, inatajwa imeshafikia lengo la pili kati ya malengo matatu ya UNAIDS 95-95-95 kabla ya mwaka 2025, ikionyesha upatikanaji wa programu za matibabu madhubuti kwa wale wanaojua hali yao ya VVU.

Ni utafiti uliofadhiliwa na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR) na msaada wa kiufundi kutoka Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) vya Marekani na ICAP katika Chuo Kikuu cha Columbia.

Hapo kuna washirika wa ndani, ipo Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)na taasisi nyingine kadhaa.

Katika uzinduzi wa Muungano wa Kimataifa Kutokomeza Ukimwi kwa Watoto Afrika, unaokutanisha mawaziri wa afya na wawakilishi kutoka nchi 12 za Kiafrika, pia wadau kimataifa uliofanyika mjini Dar es Salaam, Februari Mosi mwaka jana.

Hapo walikubaliana kuweka mipango ya kutokomeza Ukimwi miongoni mwa watoto, ifikapo mwaka 2030, chini ya usimamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na Kutokomeza VVU na Ukimwi (UNAIDS).

Ni muungano utakaofanya kazi kwa miaka minane, ikibainishwa kuwa wakati robo tatu ya watu wazima wanaishi na virusi vya Ukimwi, asilimia 76 wako katika matibabu.

Watoto nao ambao ni sawa na asilimia 52, ndio wanaopata matibabu ya dawa za kurefusha maisha na kupunguza makali ya VVU.

Takwimu za mwaka 2021 za UNAIDS, zinabainisha watoto 160,000 walipata maambukizi mapya ya VVU, kati yao asilimia 15 ya vifo vyote vitokanavyo na Ukimwi, vinaangukia kwa watoto, licha ya kwamba wao ni asilimia nne pekee ya kundi hilo linaloishi na VVU.

AFYA

DK. SAMIA NA VITA UKIMWI

# Kafikisha tiba 96% kusonga sifuri, 'mbishi' anayejitokeza unyanyapaa

**Na Mwandishi Wetu**

ILIKUWA mwezi Juni 2021, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na miezi mitatu tu madarakani, akatamka katika kikao cha Umoja wa Mataifa kilichofanyika kwa njia ya mtandao, kwamba Tanzania inaunga mkono mshikamano wa kimataifa kutokomeza Ukimwi.

Ni mkutano wa siku tatu uliotathmini maendeleo yaliyofikiwa duniani katika kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo, tangu kufanyika mkutano kama huo mwaka 2016.

Rais Dk. Samia akasema: "Ukimwi siyo tena hukumu ya kifo nchini Tanzania kama ilivyokuwa miaka 38 iliyopita. Vifo vitokanavyo na Ukimwi vimepungua kutoka elfu 64 kwa mwaka 2010 hadi elfu 32 mwaka 2020.

"Maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yamepungua kutoka asilimia 18 mwaka 2010, hadi asilimia saba mwaka 2020."

Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa wakati huo, Amina J. Mohammed, akachangia hoja kwamba hatua dhidi ya Ukimwi inafanikiwa, pale penye utashi kisiasa, mshikamano na sayansi na hata kuwezesha kuutokomeza ifikapo mwaka 2030.

Ni mkutano uliopitisha azimio la kisiasa kuongeza juhudi za kutokomeza Ukimwi duniani, Rais Dk. Samia akihakikisha inaunga mkono mshikamano huo wa kimataifa katika vita hivyo.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipomwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika mdahalo kitaifa unaohusu Ukimwi, Septemba mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

### 2022 NA UNYANYAPAA

Akihutubia Siku ya Ukimwi Duniani, katika maadhimisho kitaifa yaliyofanyika mkoani Lindi katika Uwanja wa Michezo Ilulu, Manispaa ya Lindi, Rais Dk. Samia akasema jitihada kubwa zinafanywa na serikali yake, kushirikiana na washirika wa maendeleo.

Hata hivyo akakiri, kuwapo changamoto ya unyanyapaa kwa waathirika kwamba halijafanyiwa kazi vizuri, akidokeza kuwapo mkakati wa tatu wakati huo, unaolenga kusaidia kuondoa unyanyapaa.

"Kuna jambo ambalo hatujalifanyia vizuri, nalo ni suala zima la unyanyapaa. Bado lipo na ndio maana tumekuja na mikakati hiyo ili kuondosha huo unyanyapaa.

"Safari tunayokwenda katika mkakati unaofuata ni kufikia malengo ya 'sifuri tatu' ifikapo mwaka 2030, lakini kwa mpango wetu 2026 ni kutokomeza Ukimwi kuwa sifuri na maambukizi mapya ya VVU, sifuri ya kifo na sifuri ya unyanyapaa."

Katika vita hivyo, Rais akasisitiza utekelezaji wa mpango huo ni vyema kushirikiana jamii zote na lisikabki kuwa la Wizara ya Afya pekee.

Hapo akaielekeza wizara hiyo, pia Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), kwa kushirikiana na sekta zote wadau, kuhusu mapambano hayo kuwekewa mkazo kwenye jitihada na mikakati ya kuzuia maambukizi mapya, upimaji VVU na matumizi ya dawa za kinga - ARV, ili kutokomeza vifo vyake.

### KILICHOJIRI 2023

Ulikuwa mwaka uliofuata baada ya tukio la Lindi mnamo Septemba mwaka 2023, kukawapo, tukio la 'Mdahalo wa Kitaifa Kuimarisha Ubia Baina ya Serikali, Wadau na Jamii kwa Uendelevu wa Mafanikio ya Mwitikio wa Ukimwi nchini.

Kwenye tukio hilo lililofanyika kwenye ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma, mgeni rasmi mwalikiwa Rais Dk. Samia, aliwakilishwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Hapo akasema kwamba malengo ya mwaka 2025 ni kwamba: "Leo hii (Septemba, 2023) tayari asilimia 96 ya watu wanaoishi na mambukizi ya VVU wanajua hali zao.'

Majaliwa akaendelea: "Asilimia 98 ya wanaojua hali zao wapo kwenye tiba ya ARV na kati yao, asilimia 97 wameweza kufubaza wingi wa virusi kwenye damu.

"Jukumu kubwa la taifa tulilo nalo ni kulinda na kuyaendeleza mafanikio haya kwa nguvu za pamoja na umoja hadi tufikie malengo ya sifuri tatu ifikapo mwaka 2030."

Majaliwa akafafanua kuwa serikali itaendelea kuimarisha uwekezaji na mifumo endelevu ya upatikanaji rasilimali fedha, kwa ajili ya afua mbalimbali za Ukimwi, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (Aids Trust Fund) na mipango katika ngazi ya halmashauri na taifa kwa ujumla, ili malengo ya kutokomeza ugonjwa yafikiwe.

Waziri Mkuu akawahakikishia wadau hao akiwamo Mwenyekiti wa Baraza la Watu Wanaoishi na VVU (NACOPHA), kuyafanyia maoni kazi yao ya mdahalo, akinena: "Suala la ubia halikwepeki tunatambua umuhimu wa ushirikiano na tutalitekeleza kwa maslahi mapana ya Watanzania.

"Serikali itazidi kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali waliopo nchini na nje ya nchi hasa katika uwekezaji, kutoa elimu, vifaa tiba, wataalamu, maboresho ya sera na miongozo mbalimbali ya masuala ya UKIMWI.

"Tumewasikia wadau na pia tumepata maoni kutoka kwa ndugu zetu WAVIU. Maoni haya yatasaidia kuboresha mikakati ya serikali kuhakikisha tunafikia malengo."

Anasema, licha ya utafiti kuonyesha kupungua unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya VVU nchini, bado matendo hayo na ukatili wa kijinsia yanaendelea kuwa kikwazo cha kuzifikia na kuzitumia huduma za VVU kwenye jamii, shuleni, vyuoni na sehemu za kazi.

Mwenyekiti wa NACOPHA, Leticia Moris, anasema baraza hilo limetimiza miaka 21 tangu kuanzishwa, akiishukuru serikali na wadau wa maendeleo kuendelea kuhakikisha huduma mbalimbali, zikiwamo dawa za kufubaza VVU zinaendelea kupatikana.

### OKTOBA 2024

Akiwa ziarani Geita mwezi uliopita, Rais Dk. Samia akahutubia mkutano, akinena: "Kwa upande wa VVU, nchi yetu imekuwa ikipambana na janga hilo zaidi ya miongo minne sasa.

"Kwa mujibu wa utafiti wa hali ya Ukimwi nchini, kiwango cha maambukizi ya VVU kwa watu wazima, yaani vijana kuanzia miaka 15 kwenda juu ni asilimia 4.4 kwa mwaka 2022/2023."

## Ujue ugonjwa maburg usiotibika, umefafana na Ukimwi, tofauti ni...

**INATOKA UK.11**

Dk. Jonas anasema, pale mtu anaona mojawapo kati ya dalili hizo, moja kwa moja inampa viashiria kwamba kuna dalili za ugonjwa huo hatari. Aidha, mtaalamu huyo anabainisha kwamba ugonjwa huo hauna tiba maalumu wala chanjo, mgonjwa hutibiwa kulingana na dalili zikiambatana na ugonjwa huo.

Akafafanua uwezekano wa mgonjwa kuishi huongezeka pale mtu anapopata matibabu kwa wakati kutoka kwenye kituo cha huduma za afya.

### NAMNA KUJIKINGA

Jinsi ya kujikinga nao, inatajwa ni kuepuka kugusana na mgonjwa, kama kusalimiana na kugusana.

Hiyo inaweka tahadhari ya msingi kwamba, mara zote kwa kuepuka ama kugusa au kuosha maiti ya mtu aliyefariki, akiwa na dalili za ugonjwa wa maburg.

Pia, wataalamu wanashauriwa kunawa mikono kila mara kwa maji tiririka, huku wakiacha kuchangia vitu vyenye ncha kali, vikiwamo nyembe na sindano.

Wizara ya Afya inatoa angalizo kwa wananchi ama kutomtenga au kumnyanyapaa mtu yeyote aliyeruhusiwa kutoka karantini, kwa kuwa mtu anapopewa ruhusa hiyo, ni tayari ameshathibitishwa na wataalamu kuwa hana ugonjwa huo.

Ilibainika kwamba, suala la kumnyanyapaa mhusika, linaaangukia katika tafsiri ya ubaguzi kiafya.

Mnamo Oktoba 26, mwaka huu, Wizara ya Afya ikaendeleza utoaji elimu dhidi ya magonjwa ya mlipuko nchini, kwa viongozi wa dini.

Hiyo ni hatua inayogusa utoaji elimu kwa viongozi, wafikishe elimu na ufahamu kwa waumini na jamii kwa ujumla, kupitia ngazi ya viongozi hao.

Naibu Waziri wa Afya, Godwin Mollel, ambaye kitaalamu pia ni daktari wa tiba, anasema Tanzania inapoukamata ulimwengu wa kiroho kwa binadamu, itaibuka ngazi ya juu, bila ya kupata magonjwa hayo kupitia viongozi husika.

Dk. Mollel anaitaja sayansi zote na wanasayansi wake duniani, waangukia mtazamo anaoutaja kuwa: "Dini ni jicho muhimu kutuonesha tupite wapi tusipite wapi, ili nchi iwe salama, nyinyi viongozi wa dini mmeshika ulimwengu...kupitia elimu hii naomba mkawe sikivu na nchi yetu ibaki salama."





# Muswada wapendekeza TIC, EPZA kuunganishwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUSWADA wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi wa Mwaka 2024, unapendekeza kuunganishwa kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) na kuwa taasisi moja.

Lengo ni kuondokana na mwingiliano wa majukumu na gharama za uendeshaji.

Katika mkutano wa 17 wa Bunge ulioahirishwa Novemba 8, mwaka 2024, muswada huo ulisomwa kwa mara ya kwanza kwa ajili ya hatua mbalimbali za utungaji sheria.

Kufuatia tathmini ya utendaji kazi wa mashirika ya umma iliyofanyika mwaka 2023, ilibainika kuwa majukumu yanayotekelezwa na TIC na EPZA yanashabihiana na kuingiliana.

Madhumuni ya muswada huo, yalibainisha kuwa hali hii ilisababisha mwingiliano wa kiutendaji na gharama za uendeshaji kwa serikali, hivyo ili kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wawekezaji, muswada huo unapendekeza kuundwa kwa taasisi moja itakayotekeleza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na taasisi hizo mbili.

Muswada huo unalenga kuboresha mazingira ya uwekezaji Tanzania na kuimarisha mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa uwekezaji nchini pamoja na kuimarisha masharti ya uwekezaji nchini.

**Muswada huo unalenga kuboresha mazingira ya uwekezaji Tanzania na kuimarisha mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa uwekezaji nchini pamoja na kuimarisha masharti....**

Aidha, unaopendekezwa kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022, Sheria ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje ya mwaka 2002 na Sheria ya Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ya mwaka 2006.

Pia, kuundwa kwa Mamlaka ya Kuhamasisha Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi ambayo itakuwa chombo kikuu cha serikali cha kuratibu, kuhimiza, kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji nchini na kuishauri serikali kuhusu sera ya uwekezaji.

Pamoja na hayo, muswada unapendekeza kuanzishwa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji itakayokuwa na jukumu la kutoa mwongozo na mwelekeo wa nchi katika masuala ya uwekezaji na kuidhinisha mipango na mikakati ya kuendeleza uwekezaji kwa mujibu wa vipaumbele vya nchi kwa wakati husika na kupendekeza vivutio vya ziada kwa ajili ya wawekezaji wa kimkakati.

Kadhalika, muswada unaweka masharti mbalimbali kuhusu uwezeshaji wa uwekezaji nchini ikiwamo kuwa na mfumo unganishi wa kielektroniki unaolenga kuunganisha mamlaka muhimu za serikali zinazotoa vibali na leseni mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za uwekezaji.

Aidha, ili kuwezesha upatikanaji wa ardhi inayofaa kwa ajili ya uwekezaji, muswada unapendekeza kuweka masharti kuhusu uanzishaji wa benki ya ardhi itakuwa ni kanzi data itakayohifadhi taarifa kuhusu ardhi inayopatikana sehemu mbalimbali nchini.



Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Singida, Dk. Denis Nyiraha (kulia), akizungumza na waandishi wa habari mjini Singida jana, kuhusu masuala mbalimbali ya kisiasa, ikiwemo mafanikio katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Taasisi za umma zatakiwa kutenga 30% ya bajeti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI za umma zimetakiwa kutenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi kwa ajili ya wanawake na makundi maalum, ili waweze kujikwamua kiuchumi kupitia fursa hiyo.

Naibu Katibu Mkuu wa Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Felister Mdemu aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mafunzo yanayohusu ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika ununuzi wa umma iliyoandaliwa na Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania(TWCC).

Alifafanua kuwa kutenga asilimia hizo kutawawezesha makundi hayo kunufaika na zabuni zinazotolewa na serikali pamoja na taasisi za umma na kusisitiza kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa mipango ya serikali kuhakikisha wanawake na vijana wanaongeza ushiriki na kunufaika na fursa hiyo.

Alisema wizara hiyo imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali katika kuwezesha wanawake kiuchumi nchini na TWCC ni mdau mmojawapo katika eneo la kiuchumi.

"Sote tunatambua kuwa ushiriki wa wanawake na vijana katika ununuzi wa umma bado unakabiliwa na changamoto ambazo mara nyingi hutokana na ukosefu wa utaalamu, taarifa zisizotosha kuhusu michakato ya zabuni, gharama ya upatikanaji wa mitaji pamoja na wajasiriamali wengi wadogo kuendelea kutokuwa na vigezo vya kukopesheka,"alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TWCC, Mwajuma Hamza alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuhakikisha wanawake na vijana wanawezeshwa kiuchumi na kuwafungulia milango ya fursa ndani na nje ya nchi.

# UVCCM Singida yatoa onyo kwa wanaobeza maendeleo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Singida umetoa onyo kwa watu, vyama na baadhi vikundi ambavyo vimekuwa na tabia ya kubeza maendeleo yanayofanywa na serikali.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Singida, Dk. Denis Nyiraha, alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelezea maendeleo yaliyofanywa na serikali.

Alisema hakuna sababu kwa mtu au chama kubeza mambo yanayofanywa na Serikali ya CCM.

"Nataka tuwatumie salama kama walikuwa wanafanya haya mambo kipindi cha nyuma waache, kama walikuwa wanafikiri Rais Samia Suluhu Hassan hana vijana ambao wapo nyuma yake sasa tunataka tuwaambie waache vijana tupo tumevumilia vya kutosha," alisema.

Nyiraha alisema vijana wa CCM hawatakuwa tayari kunyamaza kuona kuna genge la mtu yeyote awe ndani ya chama au nje akibainika anabeza kazi zinazofanywa na serikali.

Alisema katika utawala wa Rais wa kwanza Hayati Mwalimu Julius Nyerere alipigana mambo makuu matatu ambayo ni kuondoa umaskini, ujinga na maradhi mambo ambayo Rais Samia ameendeleza kazi hiyo kwa kuweka misingi ya uimara.

Nyiraha alitoa mfano wa maendeleo yaliyofanyika katika sekta ya elimu ni ujenzi wa shule za msingi na sekondari 3331 na madarasa zaidi ya 21,000 nchi nzima.

Alisema kutokana kuboreshwa kwa sekta ya elimu hata kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa madarasa ya awali kimeongezeka kutoka wanafunzi 1, 292,921 na kufikia 1,679 562 na kwamba kwa Mkoa wa Singida shule za msingi 673 na sekondari 183 zimejengwa.

Katika sekta ya afya kwa Mkoa wa Singida, alisema katika kipindi cha 2020 kulikuwa na maboma ya zahanati 101 lakini hadi kufikia mwaka 2024 yapo 116, vituo vya afya vilikuwa 21 lakini sasa vipo 31.





# TAKUKURU yaibua madudu miradi ya maendeleo

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani hapa imebaini mapungufu kwenye miradi mitano ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 500 na kuchukua hatua.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Mkuu wa TAKUKURU wa mkoa huo, Noel Mseo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusiana na ufuatiliaji wa miradi 33 kwa kipindi cha miezi mitatu.

Alitaja miradi hiyo kuwa ni ya sekta za elimu, afya, barabara, mifugo, maji na ujenzi wa nyumba za watumishi.

"Miradi yote ilikuwa na thamani ya Sh. Bilioni 5.4. Katika ufuatiliaji huo, mitano yenye thamani ya Sh. milioni 579,395,980 ilibainika kuwa na mapungufu na hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kurekebisha mapungufu hayo," alisema Mseo.

Alitoa rai kwa wananchi katika maeneo miradi hiyo inatekelezwa kuwa makini na kufuatilia kwa kuwa ushiriki wao ni muhimu kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

**Alitoa rai kwa wananchi katika maeneo miradi hiyo inatekelezwa kuwa makini na kufuatilia kwa kuwa ushiriki wao ni muhimu kuhakikisha inakamilika kwa wakati.**

Mseo aliwakumbusha wakandarasi, wazabuni, wahandisi, mafundi na wanakamati kutimiza wajibu wao na kutunza nyaraka za matumizi ya fedha.

Mseo alisema katika kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa wamejipanga kudhibiti vitendo vya rushwa kwa kushirikiana na wananchi, vyama vya siasa na wadau.

"Niwaombe wananchi wote kutoa taarifa kwetu pale wanapoona viashiria vyovyote vya rushwa katika maeneo yao wakati wa mchakato wa kuwapata viongozi watakaogombea," alisema Mseo.

Baadhi ya wakazi wa mjini Njombe, akiwemo Kaini Nyingu, alisema vitendo vya rushwa katika taasisi za umma havipaswi kupewa nafasi wakati wa utoaji huduma kwa wananchi.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigae (kulia), akiteta jambo na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo Vijijini (RDO), Fidelis Filipatali, wakati wa mahafali ya tisa ya Chuo cha Ufundi Stadi cha Mdabulo VTC, wilayani Mufindi, mkoani Iringa juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# SIDO yaagizwa kukopesha vyuo vya ufundi

**Na Renatha Msungu,**
IRINGA

SERIKALI imeliagiza Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kutoa mikopo kwenye vyuo vya ufundi nchini kuendeleza teknolojia ya ubunifu itakayotumiwa na wahitimu kujiajiri.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe alitoa agizo hilo wakati wa mahafali ya tisa ya Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha RDO Mdabulo yaliyofanyika jana katika viwanja vya chuo hicho kilichopo wilayani Mufindi Mkoa wa Iringa.

Kigahe, alisema ameridhishwa na bidhaa zinazotengenezwa na wanafunzi wa chuo hicho kupitia teknolojia na kwamba wakipewa mikopo midogo na SIDO watazidi kupanua wigo wa ubunifu na kuinua uchumi wao.

"Nawapongeza sana wanafunzi wa chuo hiki na wakufunzi wao kwa kubuni teknolojia hiyo, jitihada zaidi zinahitajika kutoka kwa wakufunzi wao ili wapige hatua kwa hiki wanachofanya," alisema.

Alisema ubunifu huo na elimu ya ujuzi wanayopata kutoka chuoni hapo itawasaidia kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

Alisema baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuanzisha vyuo vya ufundi stadi kila wilaya, wao kama wizara wataendelea kushirikiana nao kuhakikisha jamii inanufaika nayo kwa kujiajiri.

Alikipongeza RDO Mdabulo kutokana na fani za ufundi wanazotoa kwa wanafunzi na anaamini zinakwenda kuwasaidia kujiajiri baada ya kuhitimu masomo yao.

Vilevile, Kigae aliwataka wahitimu kwenda kutumia ujuzi waliopata chuoni hapo kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa. Katika risala ya wahitimu hao wa mwaka wa tatu iliyosomwa na Jackline Kibuga, waliiomba serikali kusaidia kuelimisha jamii umuhimu wa elimu ya ufundi stadi na kutoa kipaumbele kwa wahitimu wake.

Pia waliiomba serikali kuwaunganisha na viwanda ili kupata ajira na kuendeleza ujuzi wao.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo Vijijini (RDO), Fidelis Filipatali, aliishukuru serikali na wadau wao kwa kuhakikisha shirika hilo linapiga hatua katika kuisaidia jamii.

Filipatali, alisema lengo lao ni kuona jamii inanufaika na shirika hilo kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya elimu, maji na afya.

# Serikali yapongeza kuwatimua wanaotoa elimu kwa mtandao

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

BAADHI ya wakazi wa Halmashauri ya Manispa ya Songea mkoani Ruvuma wameipongeza serikali wilayani hapa kwa kuwatimua baadhi ya watu waliokuwa wakiendesha biashara haramu ya kutoa elimu kwa njia ya mitandao bila ya kuwa na vibali na leseni.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe juzi mjini haoa, wakazi hao, walisema kwa muda mrefu liliibuka kundi la watu na kuanzia vyuo vya kutoa mafunzo ya kutafuta masoko kwa mitandao hiyo.

Walisema mafunzo hayo yalikuwa yanatolewa katika maeneo ya Mjimwema na Msamala kwa vijana kutoka ndani na nje ya nchi.

Said Omar, Mkazi wa Mjimwema, alisema hatua iliyochukuliwa na uongozi wa wilaya hiyo kupiga marufuku vyuo hivyo na watu hao kutimuliwa inastahili kupongezwa kwa kuondoa mazingira ya utapeli kwa vijana.

Alisema vijana hao walikuwa wakishawishiwa kuwasiliana na ndugu zao wawatumie fedha za mtaji kuanzisha biashara wanazofundishwa kuzifanya kwa mtandao.

Khalfan Msoa, alisema vijana wamekuwa wakidanganyika kuwa elimu hiyo inayotolewa na vyuo hivyo itawasaidia kuondokana na umaskini na kujikuta wakiishi katika mazingira magumu zaidi baada ya kutapeliwa fedha.

Mkufunzi Msaidizi wa Chuo cha Alliance in Motion Global, Jovitha Lubida, alisema kwa muda mrefu wanaendesha mafunzo sehemu mbalimbali nchini ya kuwajengea uwezo vijana kujiajiri.

Kiongozi Mkufunzi wa QNET, Yona Maganga, alisema chuo hicho kipo kisheria na kinaendesha mafunzo kwa kufuata taratibu zilizopangwa na Wizara ya Elimu kutoa elimu kwa njia ya mtandao.

Diwani wa Mjimwema, Sylvester Mhagama, alisema katika kata yake, watu waliokuwa wakijihusisha na biashara hiyo waliondolewa, lakini anashangaa baada ya kuona baadhi wamerudi kuendesha mafunzo kwa vijana ambayo ni batili.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Wilman Kapenjama na kamati yake ya ulinzi na usalama walikwenda kwenye maeneo ambayo mafunzo hayo yanatolewa na kubaini vyuo hivyo vipo tangu mwishoni mwa mwaka jana.

Alisema amechukua uamuzi wa kuviondoa vyuo hivyo kwenye wilaya yake mpaka wamiliki wake wafuate taratibu za kisheria

Kapenjama alifafanua kuwa vyuo hivyo vinachukua vijana ndani na nje ya nchi baada ya kudanganywa kuwa kuna ajira na wakifika Songea wanalazimishwa kutoa fedha kuanzia Sh. 100,000 hadi 600,000 kila mmoja.

# Viongozi wa mashirika ya ndege duniani kukutana Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUTANO wa mashirika ya ndege duniani kwa mwaka 2025 unatarajiwa kufanyika Juni mwakani visiwani Zanzibar ambao utatoa fursa za uwekezaji na kiuchumi na kuitangaza Zanzibar kimataifa.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa Habari kuhusu mkutano huo Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohammed, alisema zaidi ya washiriki 500 kutoka maeneo mbalimbali ulimwenguni watahudhuria katika mkutano huo.

Akiwataja miongoni mwa washiriki hao alisema ni viongozi wa mashirika ya ndege ya ndani na kimataifa, viongozi wa viwanda vya ndege, wasambazaji wa huduma za usafiri wa anga, viongozi wa mashirika ya utalii, viongozi wa taasisi za serikali, wataalamu kutoka nchi mbalimbali na mashirika ya kimataifa. Alisema hiyo ni heshima kubwa kwa Zanzibar lakini pia kwa Tanzania kupata fursa hiyo adhimu kufanyika kwa mkutano huo.

Hata hivyo, alisema kuchaguliwa Zanzibar kufanyika kwa mkutano huo kutaleta fursa na faida mbalimbali ikiwemo kuitangaza Zanzibar kimataifa.

**Aidha, alisema mkutano huo ni jukwaa muhimu kwenye ramani ya kimataifa ya anga inayounganisha uhusiano kati ya wadau wa sekta kama vile mashirika ya ndege...**

Aidha, alisema mkutano huo ni jukwaa muhimu kwenye ramani ya kimataifa ya anga inayounganisha uhusiano kati ya wadau wa sekta kama vile mashirika ya ndege, viwanja vya ndege, kazi za utalii na mambo mengine. Faida nyingine alisema ni kupatikana kwa fursa za kukuza biashara na uwekezaji kupitia washiriki hao, fursa ya kuongeza maarifa kupitia wabobezi na kuiweka Zanzibar katika ramani ya kidunia.

"Mwaka 2023 Zanzibar ilipokea wageni 638, 498 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.45 ukilinganisha na mwaka 2022. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa upande wake ilipokea abiria 2,140,986 mwaka 2023 ikilinganishwa na abiria 1,773, 407 mwaka 2022 ambapo ni ongezeko la asilimia 21" alisema.

Alisema pia idadi ya mashirika ya ndege yanayofika Zanzibar yameongezeka kutoka 68 mwaka 2020 hadi 81 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 19 ambayo ni mafanikio makubwa.

Akizungumzia kuhusu Zanzibar kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo, alisema anaamini miongoni mwa sifa zilizopelekea kuchaguliwa ni sifa njema ya Wazanzibari, haiba ya visiwa, ukarimu wa watu wake, amani na utulivu uliopo na uwezo wa kutoa huduma zinazokubalika.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Seif Abdalla Juma alisema nafasi hiyo ya Zanzibar kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni heshima kubwa na fursa katika kujadili masuala ya anga na utalii duniani lakini pia kwa Zanzibar.

Alisema ZAA kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii na wadau wengine inashirikiana kwa pamoja kuhakikisha wanaleta fursa mbalimbali visiwani humo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi ya Aviadev Afrika ambayo inahusika na uandaji wa mikutano, John Cowell, alisema mkutano huo kufanyika Zanzibar utaleta hamasa ya mashirika ya ndege ya kimataifa kufanya safari zake Zanzibar jambo litakalisaidia kuendelea kuongezeka kwa soko la utalii.



Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile (katikati), akizungumza na Uongozi wa kampuni ya uwekezaji kutoka nchini China ya Foton, kabla ya kuzindua magari yake, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaingilia kati madeni ya w'biashara wa masoko

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali italifanyia kazi suala la malalamiko ya wafanyabiashara wa masoko nchini kutolipwa fedha na wamiliki wa hoteli ambao wanachukua bidhaa.

Aliyasema hayo ofisini kwake Migombani Zanzibar, alipokutana na uongozi wa Shirikisho la Umoja wa Wafanyabiashara wa Masokoni Zanzibar (SHIMAZA).

Viongozi hao walifika kwa lengo la kujitambulisha na azma yao ya kuendeleza shughuli mbalimbali ikiwemo mashindano ya michezo na usafi wa mazingira kwa maendeleo ya kibiashara kwa wajasiriamali hao.

Hata hivyo, walilalamikia pia kukosa malipo ya bidhaa zao zinazotumiwa na baadhi ya wenye mahoteli kwa muda mrefu na kuiomba serikali isaidie uwezekano wa kupata malipo yao.

Othman alisema kwamba serikali inatambua kuwepo kadhia hiyo kwa vile suala hilo liliwahi kujitokeza mwaka 2012 kwa uongozi wa iliyokuwa hoteli ya Venta Club kushindwa kuwalipa wafanyabiashara wa masoko kwa bidhaa za mboga na matunda walizozitumia.

Alisema kwamba kutokana na kujitokeza hali hiyo Serikali kupitia Mamlaka ya Ukuzaji na Uendelezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) iliweka utaratibu na mfumo maalumu wa kudhibiti hali hiyo isijitokeze tena lakini sasa imereja.

Alisema kwamba jitiada zilizofanywa na serikali wakati huo wa mwaka 2012 ilisaidia wafanyabiashara kulipwa fedha zao na kuwekwa msisitizo wa kufuatwa utaratibu na muongozo wa serikali chini ya usimamizi wa ZIPA.

Aidha, alisema wafanyabiashara wanapaswa kuzingatia usafi kwenye bidhaa zao na kuachana na utamaduni wa mazoea wa kuuza bidhaa kwa kuweka chini pamoja na mazingira yasioridhisha jambo linaloweza kuhatarisha afya ya mtumiaji.

Pia, aliwataka wafanyabiashara hao kuzingatia mifumo ya kileo ya ufanyaji biashara ambayo inauwezo wa kuongeza thamani bidhaa mbalimbali za matunda na mboga.

Wafanyabiashara hao waliomba serikali kuweka mfumo bora wa utoaji wa elimu kwa wajasiriamali waliopo masokoni ikiwa ni pamoja na kuwezeshwa kuzisindika na kuzihifadhi kwa njia za kisasa bidhaa za matunda na mboga.

# Mazrui asisitiza ushirikiano kufikia afya kidijitali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, amezitaka taasisi na mashirika ya maendeleo kuimarisha ushirikiano na taasisi za elimu ya juu, sekta binafsi pamoja na asasi za kiraia ili kufikia malengo ya mkakati wa afya wa kidijitali wa mwaka 2020-2025.

Alitoa rai hiyo juzi wakati akifungua mafunzo ya afya ya kidijitali visiwani Zanzibar yaliyolenga kujadili na kuchunguza uwezekano wa mabadiliko ya afya ya kidijitali katika kuimarisha afya na ustawi wa jamii Zanzibar.

Alisema Zanzibar imejipanga kutumia teknolojia ya kidijitali kuleta mapinduzi katika utoaji wa huduma za afya, kwa kuunda mfumo wa afya unaowezeshwa kidijitali ambao ni bora, wenye usawa na unaomzingatia huduma kwa mgonjwa.

Alisema mpango huo utawawezesha wafanyakazi wa afya ngazi ya jamii (CHWs) kutoa huduma muhimu za afya kwa kuwapa vifaa vya kidijitali vitakavyoimarisha shughuli zao ikiwemo ukusanyaji wa takwimu na zitakazosaidia kuonesha uhalisia wa maradhi yaliyopo kwenye jamii pamoja na milipuko mbalimbali inayotokea nchini.

Alisema taaluma itakayotolewa kwa wafanyakazi hao ni sehemu ya kufikia malengo ya serikali ya kuhakikisha mifumo ya takwimu na taarifa inakuwa ya kidijitali kwa lengo la kufanya maamuzi sahihi katika kufikia huduma za afya kwa wote na afya bora.

Aidha, alisema serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wananchi, wadau wa maendeleo na sekta binafsi, watahakikisha wanadumisha mpango huo ili kufikia vipaumbele vya afya vya kitaifa.

Mazrui aliishukuru taasisi ya D-tree kwa ushirikiano wao katika mipango ya afya ya jamii na uwekezaji wa afya ya kidijitali ambao umesaidia kuongeza ufanisi kwa wahudumu wa afya ya jamii na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Naibu katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Zanzibar, Dk. Mzee Suleiman Mndewa alisema kwa sasa miundombinu ya mawasiliano imeimarika, hivyo kuja kwa programu hiyo kutaendana na kasi ya mawasiliano iliyopo na kuwasaidia kufikia malengo ya watendaji hao.

Alisema ni wakati wa wahudumu kuongeza ubunifu ili kuhakikisha wanazalisha vitu vingi vitakavyoongeza tija kwenye sekta ya afya na kufikia malengo ya serikali kupitia wizara ya afya Zanzibar.

Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya, Dk. Salim Slim aliwataka wahudumu hao kuyatumia vyema mafunzo hayo sambamba na kuwataka kufanya kazi ipasavyo kwa lengo la kupunguza matatizo yaliyopo kwenye jamii ikiwemo maradhi yasiyoambukiza kama kisukari, shinikizo la damu na saratani.

Mkurugenzi wa D Tree Zanzibar, Dk. Hannah Mccarrick Mikidadi alisema kwa muda mrefu wahudumu hao wamekuwa wakisumbuliwa na matatizo mbalimbali katika utendaji wao, hivyo kufunguliwa kwa mafunzo hayo sambamba na kukabidhiwa vitendea kazi vya kidigitali kutasaidia kuifikia jamii kwa haraka.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOHN GODFREY ZAKARIA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2637/0054** kilichotolewa na **MBELEKESE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Cheti cha Chuo Certificate of Ordinary Diploma chenye namba **DSM/DPLM/20/82244** kilichotolewa mwaka 2020. Certificate of Basic Technician chenye namba **DSM/BCPLM/19/59983** kilichotolewa mwaka 2022. Vilivyotolewa na **TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTACY** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/249582/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SARAH SIMON LUVANDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3885/0067** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **WENDA HIGH SCHOOL** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIG/249277/2024.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SAMWEL JAMES FURAHISHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1910-0171** kilichotolewa na IGOMA SEC SCHOOL mwaka 2013. Cheti cha Chuo Diploma chenye namba **NS 1910/0171/2013** kilichotolewa na **EXCELLENT COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCE** mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/189527/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELLY SHADRICK NJULUMI** anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 857 AHT – LANDROVER DEFENDER 110** lenye jina la Umiliki **CHURCH OF CHRIST MISSION.** CHASSIS NUMBER: **SALLDHMF71A972805** Engine namba **16L28639A.** Yeyote atakaye iona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **PHQ/ARU/ARU/43172/2024**

## TANGAZO LA KAZI UALIMU

Tunatangaza nafasi za kazi ya Ualimu **mchepuo wa Kingereza** kwa masomo ya **Hesabu** na **Maarifa ya jamii Kuanzia chekechea hadi Darasa la saba, Sifa za Chekechea ni** certificate au diploma na kwa darasa la Kwanza hadi la saba ni Diploma au shahada ya kwanza ya elimu.

**Mawasiliamo 0783 298 900**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHABANI IDDI KUSAGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 239 ADB** aina ya **CANTER** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBA/33958/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHABANI IDDI KUSAGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 288 ADB.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/NJO/NJO/4949/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHINA PETROLEUM PIPELINE ENGINEERING COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 999 CMC.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/245572/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HUSENI ALLY NCHASI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 858 ABT.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIL/HAI/24157/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Mwanaidi Miraji Ramadhani,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Gaia yenye namba za usajili **T 194 BYU** yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI **PHQ/DOD/DOD/50667/2024**

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MUSOMA SUB-REGISTRY**

**PC CIVIL APPEAL NO. 5848/2024**

**CASE REFERENCE NO. 20240319100005848**

**( from the Decision in the Matrimonial Appeal No. 1 of 2023 in the District Court of Musoma at Musoma, originated Matrimonial Cause No. 67 of 2023 in the Primary Court of Musoma Urban at Musoma)**

**NALISIS ARCHARD NGEMELA.......................... APPELLANT**

**VERSUS**

**MARY HOSEA MAJESHI..............................RESPPONDENT**

**TO: MARY HOSEA MAJESHI**

**NOTICE FOR DELIVERY OF JUDGEMENT**

**TAKE NOTICE that EX-PARTE JUDGEMENT** in the above appeal will be delivery in by this Court on the 28th day of November 2024 at 09:30 HRS by the Honourable K.I.Kafanabo, The Judge of the High Cuort.

GIVEN under my hand and the seal of the Court this 17th day of October, 2024.

**The Deputy Registrar**
**The High Court of Tanzania**
**Musoma**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 28219/2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE NICODEMUS AMANYISYE MWAITUKA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**

**PHILEMON ANGETILE MWAITUKA........PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 4th of December, 2024.

**Dated at Kyela this 13th day of November, 2024.**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA. 99 YA MWAKA 2024**

**SHABANI ALI CHILIMA ............................................ MDAI**

**BAINA YA**

**NATIONAL MICROFINANCE BANK.............................................1 MDAIWA**
**MARTIN SHABAN KIRIA............................................................2 MDAIWA**
**YONO AUCTION MART..............................................................3 MDAIWA**
**ZAINAB JUMA HOTI................................................................ 4 MDAIWA**
**UNCLE MO ENTERPRISES.......................................................5 MDAIWA**

**KWA:**
**ZAINAB JUMA HOTI**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 15.11.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utatazi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 05 ya mwezi Oktoba, 2024.

..................................
**MWENYEKITI,**
**Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,**
**DODOMA.**

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

---

**SPECIAL RESOLUTIONS OF THE MEMBERS OF**

**POWER SHIELD COMPANY LIMITED**

**REGISTRATION NO,136968017**

At the Exdtraordinary General Meeting of the Members of POWER SHIELD LIMITED (hereinafter called the "the company" duly convened and held at the registered office of the company on 16th October,

2024, the following Special Resolution were duly passed.

1. That the Company be wound up by way of Member voluntary winding up
2. Taht MUNIR MuRTAZA DARUGAR, Director and Member of the company, is hereby appointed as liguidator for winding up the company with immediate effect

**Date this 16th day of October ,2024**

MUNIR MURTAZA DARUGAR ..........................
**(Chairman)** **(Signature)**

JONATHAN PIUS MKWAMBINA ..........................
**(Secretary)** **(Signature)**

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie, 0677 020701***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Trump amteua Musk kuongoza idara ya ufanisi wa serikali

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS mteule wa Marekani, Donald Trump, ameendelea kutangaza safu yake ya uongozi, safari hii amemteua Bilionea Elon Musk, kuwa kiongozi wa idara mpya ya ufanisi wa serikali.

Trump alimtangaza Musk, kushika nafasi hiyo ambayo atashirikiana na aliyekuwa mshindani wake katika kura za maoni kupitia chama cha Republican, Vivek Ramaswamy.

Katika taarifa yake aliyoitoa kupitia mtandao wa Truth Social, Trump alisema Musk na Ramaswamy watafungua njia kwa utawala wake kwa kuondoa urasimu wa serikali, ubadhilifu katika matumizi ya serikali, kupunguza kanuni za ziada na kurekebisha mashirika ya serikali kuu. Musk, mwanzilishi wa roboti aina ya Tesla, SpaceX na mmiliki wa mtandao wa X, alikuwa mfadhili mkuu katika kampeni ya Trump wakati wa uchaguzi mkuu

Idara ya Ufanisi wa Serikali ambayo tayari imetangazwa, itaitwa Doge kifupi cha sarafu ya mtandaoni ya Dogecoin ambayo Musk aliongoza.

Hata hivyo, taarifa ilisema idara hiyo itajiendesha kutoka nje ya serikali, na hivyo itaonekana kama chombo cha ushauri. **DW**

# Askofu Mkuu Anglikana ajiuzulu

**LONDON,** Uingereza

ASKOFU Mkuu wa Anglikana nchini Uingereza, Justin Welby, ametangaza kujiuzulu wadhifa wake kufuatia kashfa ya kuwepo kwa vitendo vya unyanyasaji wa watoto.

Uchunguzi uligundua kuwa Askofu huyo wa Canterbury mwenye miaka 68, angeweza kuripoti vitendo vya unyanyasaji uliofanywa na John Smyth kwa watoto, vijana wa kiume na polisi mnamo 2013.

Katika taarifa yake, Askofu Welby alisema kuwa ni wazi kwamba lazima achukue jukumu binafsi na la kitaasisi baada ya kuambiwa mara ya kwanza kuhusu unyanyasaji huo.

"Ninaamini kwamba kujiondoa kwangu ni kwa manufaa ya Kanisa la Uingereza." Alisema.

Aliendelea kusema "Natumai uamuzi huu unaonyesha wazi jinsi Kanisa la Anglikana linaelewa kwa uzito hitaji la mabadiliko na kujitolea kwetu kwa kina kujenga kanisa salama.

Msemaji wa Waziri Mkuu Keir Starmer alisema anaheshimu uamuzi huo ambao umechukuliwa na kuwa yuko pamoja na waathiriwa wote. **BBC**



Rais aliye madarakani, Muse Bihi Abdi

# Somaliland yafanya uchaguzi wa rais

**HARGEYSA,** Somaliland

WANANCHI wa Somaliland ambayo imejitenga kutoka Somalia, wameingia katika vituo vya kupigia kura katika uchaguzi mkuu wa rais na wabunge.

Kulingana na shirika la habari la Russia (TRT), Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa majira ya asubuhi kwa ajili ya kuwapa nafasi ya watu milioni moja wenye sifa kupiga kura.

Rais aliye madarakani, Muse Bihi Abdi, wa chama tawala cha Kulmiye, Abdirahman Irro wa chama kikuu cha upinzani cha Wadan na Faysal Ali Warabe, kiongozi wa chama cha upinzani cha UCID, wanachuana kuwania nafasi hiyo ya urais.

Upigaji kura ulianza jana saa 1 asubuhi kwa saa za Afrika Mashariki na uliendelea hadi saa 12 jioni.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Somaliland ilisema zaidi ya wapiga kura wote waliojiandikisha wanatazamiwa kushiriki katika uchaguzi huo.

Kura hiyo inakuja wakati kuna mvutano wa kikanda baada ya Somalia kupinga hatua ya Ethiopia kuchukua eneo la Somaliland iliyoko katika Bahari Nyekundu kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na uchukuzi. **TRT**




Mwanajeshi wa Kenya akiwa kwenye harakati za kuimarisha ulinzi nchini Haiti hivi karibuni. **PICHA: DW**

# Waliomtukana Rais Museveni Tik Tok wafikishwa kortini

**KAMPALA,** Uganda

RAIA wawili wa Uganda wamekamatwa baada ya kudaiwa kuwatusi familia ya Rais Yoweri Museveni, kumpitia mdandao wa Tik Tok.

Watuhumiwa hao, David Ssengozi (21) mwanzilishi wa Lucky Choice na Isaya Ssekagiri, wanatuhumiwa kumtusi Rais Museveni, mkewe Janet Museveni na mtoto wa Rais, Jenerali Muhoozi Kainerugaba.

Jaji Stella Maris Amabilis aliamuru washtakiwa hao warudishwe rumande katika gereza la Kigo hadi Jumatano ijayo kesi yao itakaposikilizwa tena mahakamani.

Katika hati ya mashtaka, washtakiwa hao wanadaiwa kutumia matamshi ya chuki na kueneza habari mbaya kuhusu familia ya rais na wanamuziki wanaohusishwa na chama tawala cha NMR.

Hata hivyo, washtakiwa hao wamekana mashtaka yao.

Waendesha mashtaka walisema kwamba waliochapisha habari hizo kwenye TikTok ambayo ililenga kukashifu, kudharau, na kueneza chuki dhidi ya familia ya Rais Museveni na watu wengine.

Hakimu aliidhinisha kuendelea kushikiliwa baada ya polisi kusema kuwa bado wanaendelea na uchunguzi.

Septemba 9 mwaka huu, msemaji wa jeshi la polisi nchini Uganda, Rusoke Kituma alionya kuacha mara moja kumtukana rais ambaye alimtaja kama alama ya heshima ya taifa hilo.

Hata hivyo, haijabainika ni ujumbe gani uliosababisha watu hao kukamatwa, lakini katika video iliyochapishwa kwenye TikTok tarehe Aprili 4, mwaka huu kwenye ukurasa wa Lucky-Choice70, wenye kichwa "maadui wangu wa kwanza", aliikosoa familia ya rais kwa kutumia lugha chafu. **BBC**

# Waziri mkuu mpya aapishwa Haiti

**PORT-AU-PRINCE,** Haiti

MFANYABIASHARAS Alix Didier Fills-Aime ameapishwa kuwa Waziri Mkuu mpya wa Haiti na kuahidi kurejesha hali ya amani na utulivu.

Fills-Aime anachukua nafasi ya Garry Conille, aliyeteuliwa mwishoni mwa mwezi Mei, lakini katika siku za karibuni alikabiliwa na shinikizo la kujiuzulu kutoka Baraza la Mpito kutokana na uteuzi wa mawaziri.

Alisema, anatambua hali mbaya ambayo nchi hiyo inapitia kwa sasa, aliahidi kuweka nguvu zake zote, uwezo na uzalendo katika kulihudumia taifa hilo lililoathirika na machafuko.

Kiongozi huyo pamoja na baraza hilo la mpito wanakabiliwa na kitisho kinachotokana na ongezeko la machafuko kutoka magenge ya kihalifu. **DW**

# UWANJA WA KMC RASMI KUFUNGWA KAMERA, TAA

**Na Adam Fungamwango**

UWANJA wa KMC Complex, uliopo Mwenge, Dar es Salaam, unatarajiwa kufungwa kamera za ulinzi kwa ajili ya usalama wa mashabiki, watumiaji na mali zao, huku pia ukitarajiwa kuwekwa taa ili baadhi ya michezo ichezwe usiku.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, juzi jioni, Ofisa Habari wa Klabu ya KMC, Khalid Chukuchuku, alisema mipango hiyo inafanywa na Halmashauri ya Kinondoni na lengo ni kuleta ufanisi, kuongeza mapato pamoja na kulinda wateja, mashabiki na mali zao.

**Chukuchuku, aliyasema hayo siku chache tu baada ya Yanga kuhamia kwenye uwanja huo, ikitoka Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.**

"Ni kweli tuna mpango wa kuweka kamera kwa ajili ya usalama wa uwanja, unajua kuna mali, na vitu vingi sana kwenye eneo lote linalozunguka uwanja wetu kwa hiyo lazima ziwekwe kwa ajili ya kuangalia usalama ili meneja aweze kufuatilia kila kitu kinachotendeka na kuendelea, kitu hiki kipo kwenye mipango ya Halmashauri ya Kinondoni, muda ukifika tutawambia," alisema Ofisa Habari huyo.

Inadaiwa moja ya sababu ambazo zimeifanya Yanga kuondoka Chamazi, ni kuwapo kwa kamera za ulinzi ambazo ni kama zilikuwa zinaingilia faragha za wateja wao.

Mbali na kufungwa kamera, Halmashauri ya Kinondoni ina mpango wa kuweka taa ili baadhi ya mechi zichezwe usiku, kitu ambacho kitaongeza mapato.

"Pia kuna mkakati wa kufunga taa ili mechi zingine ziwe zinachezwa usiku, nadhani baada ya msimu au katikati ya msimu huu jambo hili linaweza kufanyika, mashabiki wawe wavumilivu," alisema.

Uwanja huo ambao umeanza kutumika msimu huu, ulianza kutumiwa na Klabu za KMC, Simba na baadaye Coastal Union kama uwanja wao wa nyumbani, baadaye Coastal ilihama na kwenda Arusha kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Kwa sasa Yanga nayo imeongezeka KMC Complex huku uwanja huo ukiruhusu mechi zake kuchezwa mchana kutokana na kutokuwa na taa.

# *Mlandege FC, Uhamiaji kutifuana Ligi Kuu leo*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Uhamiaji na Mlandege FC, leo zitashuka dimbani kutifuana katika mzunguko wa 11 wa Ligi Kuu Zanzibar, ambayo ushindani umeongezeka tangu kuanza kudhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Katika mchezo huo utakaochezwa Uwanja wa Mau majira ya saa kumi alasiri, Uhamiaji FC inashuka uwanjani ikiwa nafasi ya nane kwenye msimamo wa ligi hiyo na alama zake 15, wakati wapinzani wao, Mlandege FC wakiwa nafasi ya pili na pointi zao 20.

Akiuzungumzia mchezo huo jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Bakari Mngazija, alisema tayari amekamilisha sehemu yake ya mazoezi na kwamba muda walioupata baada ya kumaliza mzunguko wa kumi waliutumia kufanya maboresho katika kikokosi chao hasa eneo la ulinzi na ushambuliaji.

Alisema alitumia muda mwingi katika kuhakikisha beki zote zinafanya kazi yao vizuri hasa kuzidisha umakini na mambo mengine ambayo aliyaona kwenye mzunguko uliopita

Aidha, akiwazungumzia wapinzani wao, alisema mchezo huo hautakuwa rahisi kutoka na Mlandege lengo lao ni kujiimarisha katika nafasi waliyopo mpango ambao unakwenda sambamba na Uhamiaji FC.

Alisema wachezaji wanatakiwa kujua nini uongozi unahitaji katika michezo hii iliyobakia ili kuhakikisha wanamaliza mzunguko huu wa kwanza wakiwa katika nafasi nne za juu.

"Mipango yetu ni kuhakikisha tunashinda michezo iliyobaki ili kujiweka nafasi ya juu katika msimamo wa ligi. Imebaki michezo mitano kukamilisha mzunguko huu, najua ni migumu tukianzia na huu wa kesho (leo), lakini iwapo tutakuwa na jitihada na hamasa ya kupata ushindi basi tutafanikiwa," alisema.

Hata hivyo, alisema wataendelea kuhakikisha wachezaji wanapewa hamasa kutoka kwa mashabiki wao ili kuhakikisha wanafanya vizuri uwanjani.

**JUU ZAIDI...**



Kiungo wa Simba, Augustine Okejepha, akiwa mazoezini na wachezaji wenzake katika Uwanja wa Mo Simba Arena, uliopo Bunju, Dar es Salaam, wakijiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Pamba FC itakayopigwa Novemba 22, mwaka huu, Dimba la CCM Kirumba jijini Mwanza. **PICHA: SIMBA**

# Muuaji Yanga kinara mabao 'guu' la kushoto

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Tabora United, Offen Chikola, ambaye Alhamisi iliyopita alipachika mabao mawili katika mchezo kati ya timu yake na Yanga, akiiongoza kushinda 3-1, mechi ikichezwa, Uwanja wa Azam Complex ulipo Chamazi, Dar es Salaam, anaongoza kwa kupachika mabao mengi kwa mguu wa kushoto kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi sasa.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu cha Dawati la Nipashe, mabao yote mawili aliyoyafunga kwenye mchezo huo, aliyafunga kwa kutumia mguu wa kushoto, huku moja akilifunga Oktoba 18 mwaka huu, wakati timu yake ikifungwa 4-2 na JKT Tanzania, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam.

Hii ina maana mabao yote matatu aliyofunga mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, amepachika kwa mguu wa kushoto.

Hata hivyo, mchezaji huyo haongozi peke yake kwani, straika wa Azam FC, Nassor Saadun na Ibrahim Joshua wa KenGold, nao wamefunga mabao matatu wakitumia mguu wa kushoto kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Kama ilivyo kwa Chikola, wachezaji hao wawili pia wamefunga mabao matatu kwenye ligi, hivyo mabao yote waliyonayo wamefunga kwa kutumia mguu huo.

Wakati Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama ikiwa raundi ya 10 na baadhi ya michezo ya raundi ya 11 zikiwa tayari zimechezwa, huku yakifungwa mabao 164 kwa michezo 83 iliyochezwa, jumla ya mabao 45 yamefungwa kwa kutumia mguu wa kushoto.

Wachezaji waliofunga mabao mawili kwa kutumia mguu wa kushoto kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ni Hernest Malonga wa Coastal Union, akiwa pia na idadi hiyo ya mabao, Mishano Daudi wa KenGold, Gilbril Sillah wa Azam FC na Redemtus Mussa wa KMC.

Wakati huo huo, takwimu zinaonesha kuwa, kiungo mshambuliaji Dickson Ambundo wa Fountain Gate, anaongoza kwa kufunga mabao ya faulo.

Kati ya mabao 164 yaliyofufungwa ni saba tu yaliyopachikwa kwa faulo za moja kwa moja.

Ambundo amepachika mabao mawili kwa mikwaju ya faulo, akifuatiwa na Clatous Chama wa Yanga, aliyefunga faulo moja, pamoja na Said Ndemla wa JKT Tanzania, Redemtus Mussa wa KMC, Salum Kihimbwa wa Fointain Gate na Ezekiea Mwashilindi wa Prisons.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FRIMPONG AFIKIRIWA CITY

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anafikiria kumnunua mlinzi wa Bayer Leverkusen na Uholanzi, Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 23, na beki mwenzake Mholanzi Sepp van den Berg (22), ambaye alijiunga na Brentford kutoka Liverpool msimu uliopita. ***(Football Transfers)***

### WAKALA AFUNGUKA

WAKALA wa mshambuliaji wa Canada, Jonathan David, ameziambia klabu zinazomtaka ambazo ni Juventus, Inter Milan, Liverpool na Manchester United, kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anataka mkataba wenye thamani ya euro milioni tano kwa mwaka ili kujiunga nao kwa uhamisho wa bila malipo wakati mkataba wake na Lille utakapokamilika msimu ujao. ***(Tuttosport)***

### ZIRKZEE KWA MKOPO

KLABU ya Juventus inataka kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 23, kwa mkopo kutoka Manchester United, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Tuttosport)***

### LARSSON AWANIWA ARSENAL

ARSENAL na Liverpool ni miongoni mwa klabu kuu za Ulaya zinazotaka kumuongeza kiungo wa kati wa Eintracht Frankfurt na Sweden, Hugo Larsson mwenye miaka 20, kwenye kikosi chao katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Team Talks)***

### ARAUJO ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA ni miongoni mwa klabu kadhaa, ikiwa ni pamoja na Newcastle United na Crystal Palace, ambazo zinamtaka beki wa kati wa Benfica, Tomas Araujo, 20. ***(O Jogo)***

### CARRERAS ATAJWA UNITED

MANCHESTER United imekuwa ikitafuta chaguo la kumnunua beki wa kushoto wa Hispania, Alvaro Carreras mwenye umri wa miaka 21, ambaye walimuuza kwa Benfica msimu wa majira ya joto. ***(Marca)***

### SVENSSON AIVUTIA LIVER

LIVERPOOL inavutiwa na Daniel Svensson wa Sweden, huku Manchester United na Arsenal pia wakiwa miongoni mwa klabu zinazomuwania beki huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 22. ***(Teamtalk)***

### OMORODION KUMRITHI LEWA

BARCELONA imemworodhesha mshambuliaji wa Porto, Samu Omorodion mwenye umri wa miaka 20, kama mbadala wa Robert Lewandowski wa Poland mwenye miaka 36. ***(El Nacional)***

### LAPORTE KWENYE RADA

REAL Madrid imemweka beki wa kati wa Al-Nassr ya Hispania, Aymeric Laporte mwenye umri wa miaka 30, na beki wa kulia wa Tottenham Hotspur, Pedro Porro mwenye miaka 25, kwenye rada zake. ***(Relevo)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI ATAKA KURUDI NEWELL'S OLD BOYS

**MIAMI,** Marekani

NYOTA wa Inter Miami, Lionel Messi, anataka kujiunga na timu yake ya utotoni, Newell's Old Boys ya nyumbani kwao, Argentina, baada ya kumalizika kwa msimu wa Ligi Kuu ya Marekani (MLS) wa mwaka 2025.

**Kwa mujibu wa ESPN, Messi ambaye ameshindwa kuisaidia timu yake kwenda hatua ya nusu fainali ya mtoano wa Ligi Ukanda wa Mashariki licha ya kufunga mabao 20 katika msimu huu, anachosubiria kwa sasa ni kumalizika kwa makataba wake mwisho mwa msimu huu.**

Kocha wa Miami, Tata Martino, ameonesha wasiwasi wa kuwa nyota huyo anaweza kuondoka ingawa alishindwa kuweka wazi ni lini.

> ●●● Ni kweli mkataba wake unakaribia kuisha, lakini siwezi kusema yupo hapa kwa...

"Kwa kweli sijui ni muda gani Messi anaweza kuendelea kuwa hapa, ni kweli muda wa mkataba wake unakaribia kuisha, lakini siwezi kusema yupo hapa kwa muda mfupi," alisema Martino alipokuwa akizungumzia hatma ya Messi kikosini hapo.

Miami ambayo imeshindwa kufuzu kwenda hatua ya mtoano kwa ajili ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Marekani, tayari imeshachaguliwa kuwa timu itakayoshiriki michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2025 itakayofanyika huko Marekani jambo lililozua malalamiko kwa timu nyingi pinzani za Marekani.

FIFA iliitangaza Miami kuwa itashiriki Kombe la Dunia kwa kigezo cha kushinda tuzo ya Supporter Shield inayotolewa na waandaaji wa Ligi Kuu ya Marekani kwa timu iliyofanya vizuri katika msimu wa kawaida na wao watakuwa ndio wenyeji,

Messi na timu yake wamefanya vibaya msimu huu baada ya kutolewa katika raundi ya kwanza ya mtoano na Atalanta United.

# NEYMAR UHAKIKA KUREJEA SANTOS




**SAO PAULO,** Brazil

SANTOS imejihakikishia kurejea kwenye Ligi Kuu ya soka ya Brazil mwakani na sasa inatumaini kuwa mshambuliaji nyota Neymar atarejea katika klabu hiyo ambayo pia aliichezea Pele.

Santos, ambayo ilishushwa daraja mwaka 2023 kwa mara ya kwanza katika historia yake karibu mwaka mmoja baada ya kifo cha nguli wa muda wote Pele, ilijihakikishia nafasi yake Serie A ya Brazil kwa ushindi wa maba 2-0 dhidi ya Coritiba Jumatatu usiku.

Wendel alitangulia kufunga dakika ya 20 na Romulo Otero akaongeza la pili dakika ya 41.

Rais wa Santos, Marcelo Teixeira, alisema mapema jana kwamba, atasubiri Neymar na Klabu yake ya Al Hilal ya Saudi Arabia kuamua mustakabali wao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, mkataba wake na Al Hilal unamalizika Juni mwakani.

Mwaka 2011, Neymar aliiongoza Santos kutwaa taji lao la kwanza la Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini) katika kipindi cha miaka 48.

Aliondoka katika klabu hiyo mwaka 2013 na kwenda kujiunga na Barcelona.

"Sisi tuko wazi na tuna malengo, baba yake anajua," alisema Teixeira akiwaambia waandishi wa habari katika Uwanja wa Vila Belmiro huko Santos, nje ya Jiji la Sao Paulo.

"Inabidi tusubiri kwa sababu ana mkataba."

Teixeira aliongeza kuwa Neymar atakaribishwa uwanjani Jumapili, Santos itakapocheza na CRB na ushindi utaihakikishia Santos kutwaa taji la Ligi Daraja la pili, Serie B.

# Lampard anukia Coventry



**LONDON,** England

GWIJI wa Chelsea, Frank Lampard, ameripotiwa kuwa anachukua nafasi ya kuwa kocha mpya wa Klabu ya Coventry City.

Lampard ambaye amekuwa hana ajira tangu mwaka jana alipoachana na Chelsea aliyopewa kuisimamia kwa muda mfupi, ndiye anayepewa nafasi ya kuwa bosi wa Converty kuchukua mikoba ya Mark Robins aliyefungashiwa virago Novemba 7, mwaka huu, baada ya mwanzo mbaya katika Ligi Daraja la Kwanza England.

Tovuti ya The Mirror inadai kwamba mmiliki wa timu hiyo, Doug King, amemchagua Lampard kwa nafasi hiyo ingawa hapo awali kulikuwa na jina la Kocha wa Wycombe Wanderers, Matt Bloomfield, lakini uamuzi wa kumchukua Lampard ulipitishwa kutokana na uzoefu wa kiungo huyo wa zamani wa England.

Ripoti inaongeza kuwa Lampard anaweza kuchukua nafasi hiyo kabla ya mechi ya nyumbani ya Coventry dhidi ya Sheffield United itakayopigwa Novemba 23, mwaka huu.

Kocha Robins ambaye ameondolewa katika timu hiyo alihudumu kwa miaka saba akiiongoza kupanda kutoka Ligi Daraja la Pili hadi la Kwanza na akaiwezesha pia kucheza fainali ya mtoano ya kuwania kupanda Ligi Kuu England mwaka 2023 na wakapoteza dhidi ya Luton Town.

Hivi karibuni Lampard amekuwa akihusishwa na timu mbalimbali ambapo wiki mbili zilizopita alitajwa kuwa huenda angetua AS Roma inayoonekana kusuasua tangu kuanza kwa msimu huu, pia akatajwa kuchukua mikoba ya Kocha wa West Ham, Julen Lopetegui, ambaye amekalia kuti kavu kutokana na matokeo mbaya ya timu.

Lampard ambaye amewahi kuzifundisha Derby County na Everton mbali ya Chelsea ambayo ndio aliefundisha kwa muda mrefu zaidi, katika awamu yake ya pili kama kocha wa muda mfupi wa timu hiyo aliiongoza katika michezo 11, akashinda mmoja tu, sare mbili na kufungwa nane.

# Diaz: Wengi wanaiombea mabaya Manchester City

**MANCHESTER,** England

MLINZI wa Manchester City, Ruben Dias, amesema timu nyingi zinawaombea mabaya na kutaka wapoteze kwenye mbio za Ligi Kuu England msimu huu.

Man City imepoteza mechi nne mfululizo katika mashindano yote huku mchezo wa mwisho wakichapwa na Brighton, Jumamosi iliyopita kwa mabao 2-1.

Akizungumza na BBC Sport, Dias alisema: "Ni kawaida kuwa na nyakati kama hizi hasa kwa sababu watu wengi wanataka kutuangusha na wanaombea waone tunaanguka.

"Tunakubaliana na hali hii na tunachukua kama sehemu ya changamoto ndio maana tunapenda sana kupambana. Isingekuwa changamoto kama hizi inawezekana tusingekuwa na mafanikio haya. Haya ni maisha yetu ya kila siku na tutaendelea kupambana."

Beki huyo pia alisisitiza kwamba ni mapema sana kuanza kusema kwamba wameshapoteza ubingwa kwani msimu unaendelea na kuna mengi yanayoweza kutokea.

"Bado ni mapema katika msimu na kuna mengi yatakayojiri. Sote tunajua jinsi Ligi Kuu ilivyo. Ndiyo maana tunapenda sana hizi changamoto na naamini huu utakuwa ni msimu wa kipekee."

Man City imepoteza mechi nne za michuano yote mwaka huu kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2006 na ilikuwa mara ya kwanza kwa kocha wao, Pep Guardiola, kupata kipigo cha mechi nne mfululizo katika kipindi chote cha uongozi wake.

Baada ya kupoteza dhidi ya Bournemouth, Tottenham Hotspur, Sporting CP na sasa Brighton, vijana hao wa Guardiola wanatarajia kushuka tena uwanjani kuendelea kuweka hai matumaini ya kuchukua ubingwa msimu huu Novemba 23, mwaka huu watakapokutana na Tottenham.



# YANGA: HASIRA ZETU KWA AL HILAL CAF

Na Adam Fungamwango

NAHODHA wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, amesema hasira za kufungwa michezo mwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC na Tabora United, watazimalizia kwa Al Hilal Omdurman ya Sudan, Novemba 26, mwaka huu, itakaposhuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza juzi jioni, Mwamnyeto, alisema kwa sasa wamesahau kila kitu, ikiwamo vipigo hivyo, lakini bado wana hasira moyoni mwao na wanataka kuitoa kwa wapinzani wao hao kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi.

**Alisema mara nyingi michezo ya kimataifa inakuwa ya kiufundi zaidi na si ya kukamiana kama kwenye mechi za ligi, hivyo wanaamini kuwa hasira zao watazimalizia huko, kwani moja ya malengo ambayo wamejiwekea ni kuanza vema mechi ya kwanza ya hatua hiyo.**

"Tunaendelea vizuri na mazoezi, siku ya kwanza tulianza na mazoezi ya 'gym', leo (juzi), tumeanza mazoezi ya uwanjani kujiandaa na mchezo wetu wa kwanza Ligi ya Mabingwa.

"Tunajua hatujafanya vema kwenye michezo yetu miwili mfululizo ya Ligi Kuu, lakini mashabiki wetu wasife moyo, tumeona makosa tumeanza kuyasahihisha mazoezini, nadhani hayatojirudia tena," alisema beki huyo wa kati.

Alisema tayari, Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, ameshawapa programu ya kuifanya kwa wiki nzima ili kujiweka sawa kuelekea kwenye mchezo huo.

"Hivi ninavyozungumza tunazifanyia kazi programu za mwalimu na lengo ni kushinda mchezo ili kuanza vema kwenye mchezo wa mwanzo wa hatua ya makundi, tunawasubiri na wenzetu ambao wamekwenda kwenye vikosi vya timu za taifa warudi tuwe kamili," alisema.

Yanga ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Azam, Novemba 2, kabla ya Novemba 7 kupokea kipigo kingine cha mabao 3-1 dhidi ya Tabora United jambo ambalo lilizua mtafaruku kidogo ndani ya klabu hiyo, lakini kwa sasa mambo yamekaa sawa, huku kocha Gamondi ambaye ilidaiwa huenda akaoneshwa mlango wa kutokea akiendelea na kazi kama kawaida.

Naye daktari wa klabu hiyo, Mosea Matutu, alisema mchezaji Yao Kouassi, amerejea kikosini baada ya kuwa nje kwa wiki mbili kutokana na homa, huku Aziz Andambwile na Shadrack Boka, wakiwa bado wanapatiwa matibabu.

"Tumekuwa na majeruhi kipindi cha nyuma, lakini kwa sasa wanarejea, Kouassi amerejea, yeye alikuwa na homa, alikuwa nje kwa wiki mbili ameanza mazoezi na mwenzake, Andambwile atarejea baada ya siku 10, Boka naye amekuwa na tatizo la kifundo cha mguu, yeye atakuwa nje kwa wiki mbili," alisema.

## MSUVA: STARS ITAFUZU

Na Adam Fungamwango

MCHEZAJI wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Simon Msuva, amewaahidi mashabiki wa timu hiyo na Watanzania kwa ujumla kuwa watapambana kadri ya uwezo wao kuhakikisha wanafuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazotarajiwa kufanyika nchini Morocco, mwakani.

Akizugumza jijini Dar es Salaam baada ya kuwasili, akitokea Klabu ya Al Talaba ya Iraq, anakocheza soka la kulipwa, Msuva ambaye kwa muda mrefu hakuwapo kwenye kikosi hicho kabla ya kuitwa na Kocha Mkuu, Hemed Suleiman 'Morocco', baada ya mashabiki wengi kuomba arejeshwe, amesema anaamini mchanganyiko wa wachezaji wengi vijana wenye vipaji, pamoja na wakongwe utakifanya kikosi hicho kuwa imara na kupata ushindi katika michezo miwili ya mwisho, dhidi ya Ethiopia na Guinea.

"Nimerejea tena kwa mara nyingine kuiwakilisha nchi yangu, Tanzania ninayojivunia, tuna michezo miwili muhimu ambayo itaonesha taswira ya kufuzu AFCON.

"Tunajua umuhimu wa mchezo hii, lakini mimi kwangu naona huu dhidi ya Ethiopia ndio muhimu zaidi, huu ndio utaonesha mwanga kamili wa wapi sisi tupo.

"Tuna wachezaji vijana wenye vipaji, mwalimu amewaamini, wazoefu pia tupo kama mimi Aishi Manula, Mbwana Samatta, Shomari Kapombe naye amerejea, muunganiko huu naona unaweza kabisa kufanya tufikie malengo yetu," alisema winga huyo mwenye rekodi nzuri ya mabao kwenye kikosi cha timu ya taifa.

Aliwataka mashabiki wa soka nchini kuwa nyuma yao, kuwapa sapoti na wao kama wachezaji watapambana kwa hali na mali kuhakikisha wanawapa furaha ya ushindi na kutinga fainali hizo.

"Mimi kama Msuva, nawaahidi kuwa tutafanya vizuri, wao watuamini na watuombee, sisi tutawawakilisha vizuri uwanjani," alisema.

Stars inatarajia kukikipa Novemba 16 dhidi ya Ethiopia, mechi itakayochezwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Novemba 19, mwaka huu, ikitarajiwa kukipiga dhidi ya Guinea.

Katika Kundi lao la H, Stars inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo, ambapo imejikusanyia pointi nne, DR Congo ikiongoza kwa pointi 12 na Guinea ikiwa nafasi ya pili ikiwa na pointi sita.

Timu mbili kwenye makundi yote 12, zinafuzu kucheza fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.



Viungo wa Yanga, Jonas Mkude (kushoto) na Maxi Mpia Nzengeli, wakiwa mazoezini Dar es Salaam jana kujiandaa na mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan, itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Novemba 26, mwaka huu. **PICHA: YANGA**

## Simba Queens yailiza tena Yanga Princess

INATOKA UKURASA 24

fanya mabadiliko, lakini mchezo ulionekana kupoa zaidi na wachezaji wa pande zote mbili walionekana kuchoka kadri muda ulivyozidi kusonga mbele.

Ni kipindi ambacho Simba Queens ilikosa mabao mengi ya wazi kuliko wapinzani wao.

Ushindi huo unaifanya Simba Queens kufikisha jumla ya pointi 12, ikishinda mechi zake zote nne ilizocheza, ikiendelea kukaa kileleni, huku Yanga Princess baada ya sare tatu, ikipoteza mchezo wa kwanza na kubaki na pointi tatu.

## *Simba yashtukia ya Kaizer Chiefs*

INATOKA UKURASA 24

"Simba tuna uzoefu na michezo hii ya kimataifa, kama huna utimamu wa mwili na ukikaa bila kucheza kwa wiki mbili au zaidi itakupa tabu, ndiyo maana viongozi wetu na kocha Fadlu waliiomba Bodi ya Ligi mechi yao irudishwe kwenye ratiba ya awali," kilisema chanzo ndani ya Simba.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema mchezo huo utapigwa Ijumaa ya Novemba 22, Uwanja wa CCM Kirumba, akiwataka mashabiki wengi kujitokeza kwa wingi.

Alisema mchezo huo, pamoja na kwamba ni wa Ligi Kuu, lakini utakuwa ni kama wa kujipima nguvu kuelekea katika mechi dhidi ya timu hiyo ya Angola.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Bodi ya Ligi, Karim Boimanda, alisema waliitisa michezo hiyo miwili na kusema wataipangia tarehe nyingine ili kuzipa muda timu hizo kujiandaa na michezo wa kimataifa, huku baadhi ya wachezaji wao wakiwa kwenye timu za taifa, lakini mchezo dhidi ya Simba wameupanga uchezwe Novemba 22, huku wa Yanga ukitarajiwa kupangiwa tarehe nyingine.

Michezo
Alhamisi Novemba 14, 2024
Nipashe



Lampard anukia Coventry UKURASA 22

# Simba Queens yailiza tena Yanga Princess

Na Adam Fungamwangwo

●●● Maumivu yazidi kuongezeka Jangwani, hii ni baada ya kipigo cha...

HUKU mashabiki wa Yanga wakiendelea kuugulia timu yao ya wanaume kuangukia kipigo mara mbili mfululizo kwenye mechi za Ligi Kuu Bara, timu ya Simba Queens, imepeleka kilio tena kwa wadada wao, Yanga Princess baada ya kuitandika bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara kwa Wanawake iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana.

**Yanga ilikubali kipigo kwenye Ligi Kuu msimu huu kwa mara ya kwanza ilipocheza na Azam FC na kulala kwa bao 1-0 na kisha kuchapwa 3-1 na Tabora United mechi zote zikipigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.**

Katika mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake jana, bao la kujifunga la Danai Bhobho, liliipa Simba Queens pointi tatu na kusababisha Yanga Princess kulala 1-0, katika Uwanja wa KMC Complex.

Tukio hilo linafanana na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, dabi ya wanaume, ambapo Kelvin Kijili wa Simba alijifunga mwenyewe na kuipa Yanga ushindi wa bao 1-0, mechi iliyochezwa, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Oktoba 19, mwaka huu.

Banai, kiungo mkabaji raia wa Zimbabwe aliyejiunga na Yanga Princess msimu huu akitokea Simba Queens, aliuweka mwenyewe mpira ndani ya wavu kwa mguu wa kushoto dakika tatu tu baada ya mapumziko, wakati akiokoa krosi iliyopigwa na Elizabeth Wambui ambayo ilikuwa inakwenda kumkuta Vivian Corazone.

Mchezaji huyo katika jitihada zake za kutaka kuuokoa mpira usimfikia kiungo mshambuliaji huyo raia wa Kenya, akaukwamisha wavuni.

Ushindi huo umeifanya Simba Queens kulipa kisasi cha kufungwa katika mchezo wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya kutoka sare ya bao 1-1, mechi ikipigwa kwenye uwanja huo huo Oktoba 2, mwaka huu.

Yanga Princess walianza kufika kwenye lango la Simba Queens mapema tu sekunde 20 za mwanzo katika mchezo huo wa raundi ya nne ya Ligi Kuu, shambulizi lililofanywa na Ariet Udong, lakini shuti lake lilitoka nje.



Wachezaji wa Simba Queens, wakishangilia baada ya Danai Bhobho wa Yanga Princess kujifunga kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana. Simba Queens ilishinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

Kama vile haitoshi, mchezaji huyo nusura aipatie timu yake bao dakika ya pili ya mchezo baada ya kupiga kichwa mpira wa faulo iliyopigwa na Danai, mpira ukatoka juu la lango.

Simba Queens ilijibu dakika ya nne kwa mpira wa faulo uliopigwa na Vivian, uliokwenda kutua kwenye kichwa cha Mkenya mwenzake, Jentrix Shikangwa, mpira ukatoka nje.

Katika kipindi chote cha kwanza, Simba Queens ilionekana kucheza pasi fupi fupi na kushambulia lango la Yanga Princess, ambao mabeki wake chini ya Diana Antwi walionekana kusimama imara kuokoa hatari zote.

Yanga Princess waliamua kukaa nyuma ya mpira, lakini walifanya mashambulizi ya kushtukiza kwa pasi ndefu kupitia kwa straika wao mwenye mbio, Ariet na mara kwa mara walikuwa hatari mno wanapofanya hivyo.

Kipa wa Yanga Princess, Rita Akarekor, alilazimika kufanya kazi ya ziada dakika ya 12, alipopangua shuti la Elizabent Wambui, na dakika moja baadaye alizima shambulizi lingine lililofanywa na Shikangwa.

Wema Richard angeweza kuipatia Yanga Princess bao dakika ya 20 baada ya krosi aliyopiga kukatika na kuonekana ikienda kujaa wavuni, lakini golikipa, Janeth Shija, aliruka juu na kwa ustadi alipangua na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Yanga Princess ilifanya shambulio lingine kali dakika ya 36, lakini mabeki wa Simba Queens walikaa imara kuokoa.

Kipindi cha pili timu zili-

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba yashtukia ya Kaizer Chiefs CAF

Na Adam Fungamwangwo

KIPIGO cha mabao 4-0 ilichokipata Simba, Mei 15, 2021, kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Kaizer Chiefs, ndiyo sababu iliyoifanya timu hiyo kuomba mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Pamba Jiji FC ulioahirishwa wa Bodi ya Ligi urudishwe.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zimesema kuwa uongozi wa Simba pamoja na Kocha Mkuu, Fadlu Davids, walikaa na kushauriana kuwa mchezo huo ulioahirishwa kwa ajili ya kutoa fursa kujiandaa vizuri na mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola, unaotarajiwa kuchezwa, Novemba 26, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, na kuamua urudishwe ili kuwafanya wachezaji wasikae muda mrefu bila kucheza.

Viongozi wa Simba walikumbuka kilichowapata kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya Kaizer Chiefs ambapo waliomba waahirishiwe baadhi ya michezo yao ya Ligi Kuu na kukaa wiki mbili bila mchezo wowote kitu ambacho kilichangia kufungwa idadi hiyo ya mabao katika mchezo wa kwanza uliochezwa Afrika Kusini, kabla ya kushinda mabao 3-0 mchezo wa marudiano, Mei 22, 2021, lakini hayakuweza kuifanya kutoaga mashindano hayo na kushindwa kwenda hatua ya nusu fainali, ikitolewa kwa jumla ya mabao 4-3.

Bodi ya Ligi iliahirisha michezo ya Ligi Kuu kati ya Simba dhidi ya Pamba Jiji, na Yanga dhidi ya Fountain Gate iliyokuwa ichezwe Novemba 21, mwaka huu, ili kuzipa muda timu hizo kujiandaa na mechi za kimataifa.

Yanga inajiandaa na mechi dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, Novemba 26, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002